African Journal of Advanced Social Sciences

AJASS




Open Access

Check for updates

RESEARCH ARTICLE **Section:** *Literature, Linguistics & Criticism*

# Uhakiki wa Maudhui ya Distopia Katika Riwaya Teule za Kiswahili

**Martha Nyangweso Syekei[1], Carren Nyandiba[2], & Silas Owala[3]**

[1&2]Chuo Kikuu cha Rongo
[3]Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Lugha, Fasihi na Utamaduni, Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

## IKISIRI

Fasihi kama kioo cha jamii, huelimisha, huhifadhi tamaduni za jamii na pia kuadilisha. Katika fasihi andishi vipengele vya fani na maudhui ndivyo vikuu. Utafiti huu wetu ulifaidi kutoka kipengele cha maudhui yalihakikiwa ili kuelezea mada yetu ya daistopia. Daistopia ni jamii iliyochorwa na mwandishi wa kazi ya fasihi andishi na sifa kuu ya jamii hii lengwa ni kutozingatia maadili. Utafiti huu ulihakiki utanzu wa riwaya ambao ulimulika daistopia kwa kina ili kuonyesha makuzi na maendeleo yake. Utafiti huu ulihakiki riwaya teule za Kiswahili *Kufa Kuzikana* (2003), *Dunia Yao* (2006) na *Chozi la Heri* (2014). Riwaya hizi ziliteuliwa kwa kusudi la kuafiki malengo mahsusi ya utafiti huu ambayo ni kuhakiki maudhui daistopia katika riwaya teule za kiswahili; kutathmini mtindo uliotumika katika ujenzi wa daistopia katika riwaya teule na kuhakiki mitazamo ya daistopia katika riwaya hizi teule. Ili kufanikisha utafiti huu tuliongozwa na nadharia ya Umitindo iliyoasisiwa naye Buffon (1930). Nadharia hii ilikuwa kama dira katika kuzingatia mihimili yake ili kukusanya data mwafaka kukidhi malengo ya utafiti wetu. Utafiti wetu ulikuwa wa maktabani. Data ilikusanywa na kuwekwa katika makundi matatu makuu yanayoafiki malengo ya utafiti wetu. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu elezi na matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya kinathari. Matokeo yalikuwa na mchango mkubwa katika fasihi ya lugha ya Kiswahili kwa kuwa yaliongezea maarifa kuhusu daistopia na jinsi imesawiriwa katika sanaa ya fasihi andishi katika lugha ya Kiswahili.

**Maneno Muhimu:** Mfumo, Distopia, Utandawazi, Teknolojia, Uasi

**African Journal of Advanced Social Sciences**

Volume 1, Issue 1, 2026

**ARTICLE HISTORY**

Submitted 21 December 2025

Accepted: 17 January 2026

Published: 26 January 2026

**HOW TO CITE**

Syekei, M. N., Nyandiba, C., & Owala, S. (2026). Uhakiki wa Maudhui ya Daistopia Katika Riwaya Teule za Kiswahili. *African Journal of Advanced Social Sciences, 2*(1). Retrieved from https://journals.evonexpublishers.com/index.php/ajass/article/view/60

**Published in Nairobi by Evonex Global, an imprint of Evonex Publishers Limited**

© 2026 The Author(s). This is an open Access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution License (http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/), which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium, provided the original work is properly cited.

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake. Fasihi hugusa na kuacha waja na kuwaathiri ambapo matokeo hupatikana katika maumbo mbalimbali yanayotambuliwa na jamii fulani (Wamitila, 2003). Hii inamaanisha kuwa fasihi ni ufundi ambao hutumia lugha na ina vipengele vitatu vikuu; fani, maudhui na mitazamo. Vipengele hivi vya fasihi vinasukwa na kufinyangwa na kila mwandishi ili kuuwasilisha ujumbe kwa njia teule. Ufundi huu hubainika wazi kutoka mwandishi mmoja hadi mwingine na huathiri msomaji kwa njia moja au nyingine.

Mugambi (1982) anatueleza kwamba, fasihi ni silaha katika ghala nyingi zinazotumiwa na tabaka moja kuwasilisha maslahi yake katika mapambano. Fasihi imetumiwa kama silaha katika uzinduzi wa umma mpana. Mchango wa waandishi wa fasihi kumulika masuala fulani katika jamii umechukulia kama ni vita vya kisaikolojia, hasa nyakati hizi ambapo pana harakati za ujenzi wa jamii mpya. Katika miaka ya karibuni, kumekuwa na mikataba mbalimbali inayowasilisha na kuangazia masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kupitia mashirika na maandishi mbalimbali.

Sanaa ya fasihi imekuwepo na imeendelea kukua tangu karne ya kumi na tisa. Mahsusi, maandishi ya miaka ya elfu moja mia kenda na arobaini na pia miaka ya hamsini yaliakisi ubepari, kisha baadaye yakazuka maandishi yaliyolenga ushosholisti. Katika harakati za kudhibiti jamii za kibepari na kisosholisti, propaganda ilitumika kuendeleza jamii hizo. Lengo kuu la jamii hizo zilikuwa kuonyesha maendeleo ya kijamii na kisiasa. Baadhi ya maelezo ya kitamaduni ya mfumo kamili ya utopia yaliandikwa katika historia ya Marekani katika vipindi kama vile, *Zama za Dhahabu* mwaka wa 1928 naye Morris Walter*, Nineteen Eighty Four* mwaka wa 1949 naye *George Orwell* nacho *Woman on The Edge of Time* mwaka wa 1976 maandishi yake Marge Piercy.

Mikondo ya utopia iliyoakisi masuala mbalimbali ilizuka. Mkondo wa kwanza ulikuwa wa kijamaa uliohusu watumwa na utawala wa kibepari. Mkondo wa pili wa kiteknolojia ulizuka ulioakisi masuala ya maendeleo ya sayansi. Nchi zilibuni vifaa vya kurahisisha mambo kama usafiri, viwanda na mawasiliano. Mwandishi Shaban Robert katika riwaya ya *Kusadikika*, (1973) na Katama Mkangi katika riwaya ya *Walenisi*, (2003), ni baadhi tu ya kazi zilizokuwa za utopia au hali shwari. Katika karne ya 19 na 20 neno utopia lilibuniwa bara la Uropa, katika eneo la Ugiriki ambapo lilimaanisha mahali au jamii bora. Baadaye utopia ilibadilika na kupata mipango isiyo ya kweli na upangaji upya wa mahusiano ya kijamii na kuzuka maendeleo ya sayansi kuhusu jamii, utopia ilipoteza jukumu lake. Upangaji upya wa mahusiano ya kijamii, pamoja na ujio wa utandawazi na athari zake ndipo daistopia ikazuka.

Kulingana na Mukobwa, (1987), wasanii hudhihirisha vipawa vyao kwa namna tofauti tofauti. Waandishi wa kazi za daistopia wana imani kwamba matatizo yanayowakabili wanajamii yanaweza kumulikwa, kukashifiwa na hata kutatuliwa. Waandishi hawa huwa wa kimapinduzi. Huwa na ndoto ya kuwa na jamii mpya inayowahimiza watu katika harakati za kujiendeleza na kujikomboa. Kwa maoni yetu, usomi na kuelezea wanagenzi dhana mpya ni maendeleo katika sekta ya elimu na hivyo basi juhudi za waandishi ni za kushabikiwa na kuenziwa.

Daistopia ikawa ni jamii iliyovunjika, isiyopendeza au katika hali iliyokandamizwa au ya kutisha. Hali inayosawiriwa ikawa mbaya, iliyojaa giza na isiyo na matumaini. Kazi zilizobuniwa kuelezea daistopia zilibuniwa kufichua hofu kuu ya jamii. Serikali ya kiimla hutawala na mahitaji ya watu binafsi yanakuwa chini ya serikali. Katika riwaya nyingi za daistopia, serikali dhalimu hujaribu kukandamiza na kudhibiti raia wake kwa kuchukua ubinafsi wao.

Kipindi cha baada ya miaka ya kati ya 1960 kilitoa riwaya zilizo na sifa mbili kuu. Sifa ya kwanza ikawa ni juhudi kuu ya kutafsiri hasa riwaya za Kiingereza katika Kiswahili. Sehemu kubwa ya riwaya hizo zilijumuika katika mkondo wa fasihi ya Kiswahili. Mtaalamu Kitula, 1999 anasema kuwa riwaya zilizotafsiriwa zimeikwasisha fasihi ya Kiswahili kwa kuiboresha mitazamo na mielekeo yake kwa kuipanua mipaka ya maudhui na maswala yake. Sifa ya pili ilikuwa ni kazi zilizotungwa na zikawa fasihi yenye msimamo wa Kiitikadi. Jamii ilichambuliwa kwa undani zaidi kwa kuhusisha mbinu za kisayansi za uchambuzi. Wakati huu kukazalika riwaya za fasihi ya kisasa. Baadhi ya riwaya za kisasa ndizo zilizobuni kazi zilizotalii dhana ya daistopia. Baadhi ya riwaya hizo zilijenga taswira mpya ya kukosoa utopia, kazi hizo ndizo tutazihakiki kubaini dhana ya daistopia. Daistopia ilitabiri mustakabali mbaya kwa wanadamu na kuonya juu ya hatari ya 'kuwafurahisha watu'. Kipindi kati ya mwaka 2003 hadi 2014 kilisheheni maendeleo makubwa ya kisayansi. Maendeleo haya ya kisayansi nayo yakazua athari katika jamii iliyojaa uozo na uovu. Ni katika ari hii ambapo tulihakiki mitazamo, fani na maudhui katika kila riwaya kama vipengele vya fasihi vilivyosaidia kumulika suala la kidaistopia. Kazi za hawa waandishi tofauti zimeijenga dhana ya daistopia kwa njia teule.

### 1.1. Nadharia ya Umitindo

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umitindo. Nadharia ya Umitindo imeasisiwa naye Buffon (1930). Kulingana na Buffon mtindo ni 'mtu mwenyewe'. Hii ina maana kuwa ni ule upekee wa mtu katika matumizi yake ya lugha ili kuwasilisha ujumbe wake.

Mtindo ni dhana yenye utata kuieleza. Msokile (1993) anaifafanua dhana ya mtindo kwa njia mbili. Kwanza, ni namna ambavyo mwandishi ameipa sura kazi yake kifani na kimaudhui na kuitofautisha na nyingine iliyoundwa na mwandishi mwingine. Aidha, anadai kwamba kile kinachoelezwa kinaweza pia kuitwa mtindo. Madai haya yanatiwa nguvu na Ngara (1981), anayeeleza mtindo kuwa ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha; yaani ni jinsi msemaji awasilishavyo ujumbe wake.

Kwa kuchangia dhana ya Umitindo, Crystal na Davy (1969:10) wanasema hivi:

> *Lengo la Umitindo ni kuchanganua tabia za lugha kwa kubainisha sifa mahsusi zilizobanwa katika miktadha maalum kutoka kwa sifa za kijumla za kiisimu ambazo hupatikana katika kila muktadha wa matumizi ya lugha. (TY)*

Miongoni mwa waitifaki muhimu wa nadharia hii ni Coombes (1953), aliyesema kwamba:

> *"Mhakiki ni lazima azingatie vipengele vinavyofanya kazi fulani iwe ya kuvutia. Nia ya mtindo ni kuchunguza na kuchanganua lugha na kaida zake kwa nia ya kutambua mbinu zilizotengwa kwa kazi fulani ya kijamii, kufafanua sababu ya vipengele fulani kutumiwa na vingine kuachwa."*

Kwa mujibu wa maelezo haya ni wazi kuwa nadharia ya Umitindo hujishughulisha na namna ya msanii alivyoitumia lugha katika kuwasilisha ujumbe wake. Madai haya yanaungwa mkono na wataalamu wengi katika fasihi wakiwemo (Senkoro, 1982; Wamitila, 2013 na Mosha, 2002). Wataalamu hawa wanakubali kuwa maana ya kazi ya fasihi hujikita katika mtindo alioutumia mwandishi katika matini husika. Maelezo haya yalisaidia kuchanganua matumizi ya lugha kidaistopia katika riwaya teule.

Nadharia ya Umitindo huhusisha maelezo ya kiisimu ili kuweza kufafanua dhana zake za kimsingi katika fasihi. Maelezo ya Leech (1969) kuhusu uhusiano uliopo baina ya fasihi na isimu yanaonyesha kuwa dhana hizi zinakamilishana katika utendaji kazi. Anasema hivi:

> *Uhakiki wa mtindo hauhusiani tu na ufasiri wa maana za matini kwa mtazamo wa kiisimu. Nadharia hii kama taaluma haijisimamii pweke bali huhusisha vipengele vya kifasihi na vile vya kiisimu katika uhakiki. Hii ni kwa sababu ya ugumu uliopo katika kuufafanua msamiati mpana wa kimsingi wa kihakiki katika fasihi kama vile sitiari, taswira, kijembe, kinaya, usambamba na jazanda bila kurejelea dhana ya kiisimu. Hivyo basi kwa kuziunganisha taaluma hizi mbili – ya fasihi na ya isimu kiutendaji, nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo inakuwa jukwaa la kushughulikia dhana za fasihi na isimu kwa pamoja. (uk. 2) (TY)*

Kimsingi, Leech anaashiria kuwa uhakiki wa mtindo huhusu kuchanganua vipengele vya fasihi na pia vile vya isimu. 'Hakuna kipengele mojawapo kati ya fasihi na isimu ambacho kinaweza kusimama pweke na kujifafanua kikamilifu'. Hii ni ishara kwamba nadharia ya Umitindo hutumia maelezo ya isimu na fasihi katika kufafanua matini mbalimbali. Hii ina maana kuwa kila tunapohakiki mtindo katika mkabala wa kifasihi hatuwezi kupuuza matumizi ya vipengele vya kiisimu pia.

Mtaalamu Indagasi (1988), anaunga mkono maelezo ya Leech anaposema kuwa nadharia hii hujihusisha na jinsi lugha ilivyotumika kuleta mvuto kisanaa. Mhimili huu utatufaa katika kuchanganua fani za mwandishi kidistopia na kuonyesha mbinu za usimulizi zilivyochangia katika riwaya tulizoziteua. Leech, anaeleza kuwa lengo la nadharia ya Umitindo ni kuchunguza lugha na kanuni zake ili kubainisha mbinu zilizotengewa kazi fulani ya kijamii. Leech anaonekana kusisitiza kuwa nadharia ya Kimtindo hudhamiria kufanikisha uchunguzi wa kina wa matumizi ya lugha katika fasihi. Fani hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ili kusaidia kuwasilisha ujumbe wake. Mhimili huu ulitusaidia kuchanganua lengo la kwanza lililohusisha maudhui ya daistopia katika riwaya teule za Kiswahili.

Lugha ndicho chombo tekelezi kinachosaidia kuelewa ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi. Maoni haya yanaungwa mkono na Tunner (1973), anaposema kuwa uteuzi wa maneno si huru na msanii hulazimika kuwa makini ili kazi yake ikubalike na walengwa au hadhira yake. Matumizi ya lugha huathiri maana. Mhimili huu ulitusaidia kupambanua lengo la tatu ambapo tulipambanua mtazamo wa mwandishi na msomaji kuhusu daistopia katika riwaya teule za Kiswahili.

Mwandishi hutumia lugha kiufundi na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya kisanaa katika kazi yake. Maoni ambayo yanaungwa mkono na Simpson (2004) anayedai kuwa nadharia ya Umitindo husisitiza wazo kuwa kila kazi ya fasihi ina ubunifu fulani ambao unapochanganuliwa kwa undani husaidia uelewekaji wa undani wa matini za fasihi. Pamoja na maoni haya, ni yale ya Chapman (1982) anayeelekea kuafikiana na Leech kuhusu jambo hili anapodai kuwa fasihi haiwezi kujadiliwa pasipo kuzingatia kwamba ina matumizi maalum ya lugha. Mhimili huu ulitufaa utafiti wetu kutathmini maudhui kidaistopia katika riwaya teule.

Leech na Short (1981) wameainisha viwango vya kushughulikiwa katika mtazamo wa kifasihi na ambao tutaegemea katika utafiti huu. Hivi ndivyo viwango ambavyo mhakiki anayechukua mkabala wa kifasihi huweza kushughulikia. Kwanza, ni kiwango cha kileksia ambapo aina mbalimbali ya maneno huchunguzwa kama vile nomino, vivumishi, vitenzi, vielezi na kadhalika. Pili, ni kiwango cha kisarufi ambapo aina za sentensi, uchangamano wa sentensi, aina za virai kama virai nomino, virai vitenzi na kadhalika hushughulikiwa. Tatu, ni kiwango cha kisemantiki ambapo tamathali za usemi kama vile jazanda, chuku, tashbihi na kadhalika hushughulikiwa. Nne, ni mshikamano na mwingiliano wa kimuktadha ambamo dhana za kimtindo huchunguzwa katika mwingiliano wao. Utafiti huu utahusisha kiwango cha tatu na nne ili visaidie kuhakiki daistopia kifani na kimaudhui. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na mwanamitindo Leech (1969), mihimili teule ya nadharia hii ilitusaidia kuchunguza daistopia kimtindo pamoja na kuafiki malengo ya utafiti huu.

### 2.0 Uhakiki Wa Maandishi

Hapa tutaangazia maoni ya waandishi na wataalamu mbalimbali ambao wameshughulikia daistopia. Tutaonyesha namna maandishi haya yanavyohusiana na kutofautiana na utafiti tunaokusudia kuufanya. Katika kurejea mada za kazi hizi, tulizingatia mada zenye vipengele vinavyohusiana na utafiti wetu, hasa kwa kutumia malengo yetu mahsusi ya utafiti.

### 2.1. Asili ya Daistopia

Daistopia imegawanywa katika ulimwengu mbili. Mwanzo ni ulimwengu ambapo maisha 'bora huundwa' na pili ni ulimwengu wote ambapo kila mmoja ana kizuizi cha bandia ambacho hakiwezi kushindwa. 'Dunia bora' ambayo wengi wa wahusika katika daistopia huishi imefanikiwa kwa msaada wa teknolojia na madawa ya kulevya. Nafsi ina uwezo wa kudhoofisha misingi na kuharibu 'ulimwengu bora'. Wahusika wakuu katika huu ulimwengu ni binadamu na jamii yake. Binadamu hapa huchukuliwa kuwa kitu kisichozidi, kisichohitajika na chenye madhara yasiyoendana na jamii yake.

Mollie (2003), daistopia ni mwitikio wa mabadiliko katika jamii hasa mahusiano ya kijamii katika hadithi inayofurahisha. Ni uzao wa safu mpya ya fasihi nzuri ya karne ya ishirini, ambayo ilitolewa kuwakilisha utabiri mbaya wa siku zijazo. Nafasi ya mwanadamu imehujumiwa na ubabe wa serikali dhalimu. Maafa na madhila dhidi ya wanajamii umekolea. Nguvu za kidkteta na woga husheheni jamii hizi na kutawala watawaliwa. Daistopia ni jamii yenye sifa ya kuzingatia kile ambacho ni kinyume na maadili ya mwandishi, kama vile umasikini mkubwa, kutoaminiana kwa umma na tuhuma, serikali ya polisi wakatili na ukandamizaji wa wananchi kwa ujumla. Kila kitu ni kibaya zaidi. Propaganda, woga na udhibiti wa binadamu kwa matumizi ya teknolojia huwa ndizo nguzo zinaoongoza jamii hizi. Maovu ya kijamii huathiri wote lakini wanajamii huyafumbia macho 'ni hali ya maisha' (*Oxford Dictionary,* 1978).

*(Merriam Webster's Collegiate Dictionary,* 2010), inaeleza kuwa daistopia ni hali au jamii dhahania ambayo wanajamii wanaishi katika hali mbovu zenye hatari kubwa na kwa woga wingi. Tangu enzi ya mwisho ya 'Cold War', waandishi (Bradford, Mallan, Stephens & McCallum, 2003) wanasema kuwa siku zijazo huenda zikawa na majanga makubwa. Majanga haya ni pamoja na utata wa utunzi wa mazingira na athari mbaya zaidi kuwa uharibifu wa mazingira usioweza kurekebishwa.

Mwishoni mwa mwaka wa 1890*, HG Wells*, *Ray Bradbury* na *George Orwell* wamewapa wahusika wachanga majukumu makuu katika kazi zao zinazodhihirisha daistopia. miaka ya 2000, riwaya nyingi zilibuniwa kwa lengo la kuhifadhi hali mbaya na giza lakini wahusika wakabadilika. Wahusika hapa wakawa sio raia wa kawaida na wasio na nguvu lakini vijana ambao wamewezeshwa, wasio na woga, wenye nguvu na waliodhamiria kutafuta njia za kuishi yenye ushawishi ambayo serikali dhalimu hujaribu kuwadhibiti lakini haziwezi.

Masimulizi ya daistopia hutoa somo kwamba hatua kali za kisiasa zinaweza kuwa jibu halali kwa kutokuwa na haki. Vyombo vya habari na teknolojia huwa na mchango mkubwa katika harakati za uvinjaji wa asasi za kijamii. Hadithi za kidistopia hutoa picha ya matumizi ya nguvu zaidi kutoka kwa watawala na uwezekano wa ukosefu wa haki na mabadiliko ya hewa hadi uvumbuzi wa kidikteta ulimwenguni. Zaidi, kueneza kwa masimulizi ya daistopia kunaweza pia kuhamasisha maoni ya kimawazo. Mchakato wa kihistoria katika daistopia umegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni ule utambuzi wa bora. Sehemu hii ni ya awali katika kila asili ya jamii. Sehemu ya pili husheheni majanga, mapinduzi na inajanibisha matukio kwa wakati na nafasi. Sehemu ya tatu, ni baadaye kabisa na hapa wanajamii ' hukubali' na kuishi kwa madhila, ukandamizaji na udikteta.

Hivyo basi, daistopia ni hali ya waandishi kuonyesha jinsi jamii inavyojaribu kujificha kutoka kwa ukweli wa maisha au ulimwengu wanamoishi. Kuna njama ya kina kuonyesha hali ilivyo mbaya. Kuna mgongano wa mawazo hasa baina ya wahusika ambao huzua migogoro mbalimbali. Migogoro hiyo huzua fujo na ghasia na kuna hali ya 'kujidanganya kuwa hayo ndiyo maisha'.

#### 2.1.1 Maandishi Yaliyolenga Maudhui Katika Fasihi

Maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumziwa na mwandishi. Maudhui hujumlisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mwandishi au msanii kutunga na kuisanifisha kazi yake kifasihi. Vipengele vya maudhui ni pamoja na dhamira, migogoro, falsafa na ujumbe. Wataalamu wafuatao wametafitia maudhui lakini utafiti wetu ni tofauti na wao jinsi tulivyodhihirisha.

Msomi Kurtz (1970), katika utafiti wake *Urban Obsessions, Urban Fears: The Postcolonial Kenyan Novel* anaangazia kukua kwa riwaya ya kisasa kwa kurejelea jiji la Nairobi na kulichanganua kwa kina kati ya miaka ya sabini hadi tisini akiongozwa na nadharia ya Usasa. Katika utafiti wake, mtafiti huyu aliangazia maudhui ya ukosefu wa miundomsingi, ujangili, ukahaba, familia za mitaani na biashara ndogo ndogo haramu. Utafiti wetu ni tofauti maana unaonyesha maisha ya jamii pindi tu baada ya kujinyakulia uhuru miaka ya 1960 na baadaye kabisa wakati utandawazi umekolea mwaka wa 2014. Utafiti huu ulitufaa katika maelezo ya kujadili maudhui ya kidaistopia na amehusisha riwaya jinsi tulivyofanya. Nadharia iliyotuongoza ni Umitindo.

Naye Chacha (1980) alihakiki ushairi wa Abdilatif katika kiwango cha maudhui, akizingatia *Sauti ya Dhiki* na *Utenzi wa Adamu na Hawaa* Chacha alitumia mtazamo wa Kimaksi katika kazi yake. Utafiti wake ulilenga kuibua maudhui, hata hivyo aliishia kuhakiki vipengele mbalimbali vya mtindo kwa sababu ni vigumu kutenganisha mtindo na maudhui (Masinde 1992). Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulishughulikia

maudhui ya daistopia katika riwaya tatu teule kwa kuongozwa na nadharia ya Umitindo.

Kitsao (1982) amejadili maudhui mbalimbali yapatikanayo katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Alizihakiki riwaya akitumia uchambuzi wa kitarakimu. Ameonyesha kuwa kila mwandishi huwa na jinsi teule anavyowasilisha ujumbe wake na anaweza kunasibishwa na motifu yake. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa umeshughulukia maudhui kwa ujumla nasi tulihakiki maudhui ya daistopia katia riwaya za kisasa.

Njogu (1987), katika tasnifu yake alichambua maudhui ya mapinduzi katika riwaya tatu za Kiswahili ambazo ni: *Utengano, Dunia Mti Mkavu* na *Asali Chungu.* Msomi huyu amebainisha kwamba matukio ya kihistoria huathiri jamii pakubwa. Sekta tatu kuu za kijamii, kisiasa na kiuchumi zilipelekea kutokea kwa mapinduzi visiwani Zanzibar katika mwaka wa 1964 akiongozwa na nadharia ya Uamali. Taarifa ya tasnifu ya Njogu ilitufaa maana utafiti wetu unaangazia maendeleo ya daistopia kutoka mwaka wa2003 hadi 2014. Hata hivyo, tofauti na utafiti wetu ni kuwa tulichunguza maudhui ya kidaistopia na tuliongozwa na nadharia ya Umitindo.

Naye Senkoro (1988) alihakiki maudhui katika mashairi ya watunzi mbalimbali akiongozwa na nadharia ya Umaksi. Katika utafiti wake alishughulikia vipengele vya kimtindo jinsi vinavyofanikisha uwasilishaji wa mawazo ya msanii. Aidha, alionyesha jinsi msanii anavyousuka mtindo ili kuipa kazi yake sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwingine asingeweza kuipa hata kama jambo linalozungumziwa na wasanii hawa ni lile lile moja. Utafiti wetu ni tofauti kwa vile tulishughulikia utanzu wa riwaya tukiongozwa na nadharia ya Umitindo kuhakiki maudhui ya daistopia.

Kahinde (1998), alitafitia kutamauka katika riwaya ya lugha ya Kiingereza za Meja Mwangi. Utafiti wake ulilenga kuonyesha matokeo ya ukoloni katika jamii. Mambo maovu kama chuki, woga na ukandamizaji. Nadharia alizozitumia mtafiti huyu ni za Uhalisia na Usasa. Utafiti wetu ulikuwa tofauti na huu kwa kuwa tulihakiki riwaya teule za Kiswahili na tuliongozwa na nadharia ya Umitindo.

Odhiambo (2010), alitafitia utovu wa maadili katika watoto na alihakiki riwaya tatu za Kiingereza za waandishi John Kiriamiti, Meja Mwangi na John Kiggia akitumia nadharia ya Usasa. Mtafiti huyu anaonyesha jinsi jamii za ukoloni hazikuwajumuisha watoto kama wahusika wakuu katika jamii. Athari ya kutowahusisha watoto inaleta madhara na maangamizi makuu baadaye. Tofauti na huu wetu ni kuwa tuliangazia jinsi waandishi Walibora, Mohamed na Matei wametalii mtazamo wa daistopia kwa kuongozwa na nadharia ya Umitindo kwa kuegemea utanzu wa riwaya za Kiswahili.

Bibiana (2014), amefanya utafiti kwa kuhakiki masuala ambayo yanahusu siasa ambapo anarejelea riwaya mbili za Shaaban Robert, *Kusadikika* na *Kufikirika*. Bibiana alikuwa na lengo kuu la kutathmini masuala ya kisiasa. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa viongozi walijali mahitaji yao – maudhui makuu yakiwa ufisadi na dhuluma - na kupuuza yale ya jamii pana. Mtafiti huyu aliongozwa na nadharia za Dhima na Kazi na Semiotiki. Utafiti wetu ulikaribiana na huu kwa sababu ulihusisha riwaya za Kiswahili na nadharia ya Umitindo. Tofauti ni kuwa masuala tuliyoyashughulikia ni ya kidaistopia katika riwaya teule za Kiswahili tofauti.

Osango (2015), Mtafiti huyu alieleza kuwa jamii ya Zanzibar iliathirika na ubepari ulioanzishwa na wakoloni. Hali ya ubepari ilisababisha hali ya kiuchumi kuwa mbaya. Kimsingi, alichambua ukombozi wa kisiasa na kiuchumi akirejelea riwaya ya Kiswahili *Mkamandume* akiongozwa na nadharia ya Uhalisia wa kijamii. Maudhui mahsusi aliyoyamulika yalikuwa umaskini kama athari ya siasa mbaya. Ukaribu ni utanzu wa riwaya, hata hivyo utafiti wetu ni tofauti kwa mada kwa kuwa tulihakiki riwaya teule za Kiswahili ingawa tulilenga maudhui kidaistopia na tukiongozwa na nadharia ya Umitindo.

Mtafiti mwingine ni Kinoti (2015), ambaye alitafitia mwanasiasa wa Afrika katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili. Mtaalamu huyu alitumia nadharia mseto kama zetu ilhali zake zikiwa za Ulimbwende na Baadaukoloni kuchunguza mwanasiasa wa Afrika ambapo alichukulia sauti ya mshairi kuwa sauti ya mwananchi. Tofauti nasi ni kuwa, tulitafiti utanzu wa fasihi; riwaya za Kiswahili tukiongozwa na nadharia ya Umitindo.

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tulichunguza daistopia inavyojengwa kimaudhui, kimtindo na kimtazamo katika riwaya za *Kufa Kuzikana, Dunia Yao* na *Chozi la Heri.* Waandishi hawa watatu walifaulu kutuonyesha jinsi mambo haya matatu yalivyojitokeza kwa kufinyanga kazi yao kwa kuvihusisha vipengele vya kifasihi kama vile wahusika na mandhari. Maudhui yalijitokeza kwa njia ambayo daistopia iliwekwa wazi na kwa miktadha ifaayo. Katika mtindo, aina mbalimbali ya mitindo ilichanganuliwa iliyolenga kujenga daistopia. Hatimaye, mitazamo ilihakikiwa kwa kuielezea daistopia kwa kina. Maelezo na mifano mahsusi vilitolewa ili kufikia madhumuni ya utafiti wetu. Uchanganuzi wa kina ufuatao ni idhibati ya utafiti wetu.

## 3.1 Maudhui ya Daistopia katika Riwaya Teule za Kiswahili

Maudhui ni jambo liongelewalo, uchaguzi wa jambo la kulishughulikia katika kazi za fasihi linalofinyanga madhumuni ya mwandishi au msanii aiundaye kazi hiyo ya fasihi. Kwa hiyo basi, maudhui ya kazi za fasihi hujumuisha mawazo na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mtunzi au msanii kutunga na kusana kazi fulani ya sanaa. Haya mafunzo yalihusishwa na hali halisi za kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi zilizopo katika mfumo wa jamii. Waandishi wa kazi za distopia walikuwa na malengo mahsusi ili kuweka mafunzo yao katika kazi za fasihi.

Riwaya za daistopia zinaangazia maudhui yanayohusiana na hali mbaya ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni katika jamii ya baadaye iliyoharibika. Maudhui tuliyoyahakiki yalitumika kama onyo kuhusu mwelekeo ambao jamii inaweza kuelekea. Maudhui yalichangia katika kuunda picha ya ulimwengu wa daistopia yakionyesha athari za udhalimu wa kijamii, udhibiti wa kisiasa na matumizi mabaya ya teknolojia. Matokeo yakawa kuporomoka kwa jamii kwa kukosekana umakinifu. Yafuatayo ndiyo maudhui tuliyoweza kuyaelezea kwa kina:

### 4.1.1 Udhibiti wa Serikali na Mfumo wa Ukandamizaji

Serikali au kikundi chenye nguvu kinadhibiti kila kipengele cha maisha ya raia, ikiwa ni pamoja na mawazo yao, tabia zao na hata hisia zao. Udhibiti huu unapatikana kupitia propaganda, ufuatiliaji karibu na sheria kali za kidikteta. Mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii inatumika kunyanyasa na kudhibiti watu kwa nguvu. Suala la ufisadi ni jambo ambalo linazuia kuendelea kwa jamii.
Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* Akida ni mhusika aliye mbioni kuonyesha jinsi ufisadi unakolea na kuwafaidi wa tabaka la juu kiuchumi. Akida anasimulia:

> *Nimehuzunishwa mno na visa vingi vya majengo yaliyojengwa na kusanifiwa vibaya katika miji mingi nchini, yakiporomoka na kuwaua watu bure bila kisa. ...Nikidhani ufisadi ndio hupelekea kuwepo majengo yasiyofikia viwango vitakiwavyo kujengwa mijini. (uk. 48)*

Ufisadi umeshamiri katika ofisi na asasi muhimu serikalini na unatumiwa kusahihisha hiyo mitihani na kuwapa wanafunzi alama zisizofaa kwani wana uhusiano wa karibu na wenye vyeo. Mwanafunzi aliyeibuka nambari moja; Regina Kato alikuwa mpwa wa Waziri wa Elimu. Naye Donald Kitenge aliyeibuka nambari mbili alikuwa mtoto wa mfanyakazi wa ngazi za juu katika Baraza la Mtihani wa Taifa (BMT) (uk. 51)

Mwandishi anatueleza jinsi serikali na Msomaji wa Sauti ya Kiwachema alivyobwabwaja propaganda badala ya kusema ukweli kuhusu hali ya usalama pale Baraki. Kwa bahati nzuri Tim alifajiri idhaa ya Kiswahili ya BBC iliwatangazia akina Akida habari za kutamausha:

> *"...Serikali ya Kiwachema imepiga marufuku wageni na waandishi wa habari – wa nje na wa ndani pia – kuzuru eneo la mapigano. Wadadisi wa mambo wanasema, ingawa makabila hayo mawili yamekuwa na chuki baina yao, huenda vita hivyo vimechochewa na watu wenye ushawishi mkubwa kisiasa.mapema wiki hii wahariri wakuu wa magazeti mawili nchini Kiwachema walitiwa nguvuni baada ya kuchapisha habari za vita hivyo. Matoleo ya Jumatano ya magazeti nchini humo yalinaswa yote na polisi..." (uk. 60-61).*

Serikali inadhibiti vyombo vya habari na hata matangazo ya eneo na hivyo kuwazuia raia kupata habari za Baraki. "Mkuu wa Wilaya ya Korosho...Bwana Erastus Adaulo amevishutumu vyombo vya habari vya kigeni kwa kupiga chuku hali ya usalama wilayani..." (uk. 61)

Katika Hospitali ya Rufaa ya Tandika, Tim na Akida wanasaidia kumsogeza mgonjwa mmoja kutoka eneo paa lilikuwa linavuja. Baadaye Akida anagundua ni Mzee Uledi aliye Mkanju. Mzee Uledi anaeleza madhila waliyoyapitia siku chache zilizopita; ubakaji, mauaji, majeruhi, makazi kuchomwa na sasa kuwa wakimbizi. Zaidi anaeleza kuwa vita hivyo vinaongozwa na viongozi walio serikalini na asasi zingine kama polisi:

> *"Wanaongozwa na yule mbunge wao Johnstone Mabende. Nasikia wakubwa wanamsikiliza sana, uongo wake unaaminiwa mno serikalini. Sasa Wakorosho wanataka watutimue tuwaondokee Korosho. Mara biashara yetu inaipiku yao, tuna uchawi. Mara kilimo chetu kina tija zaidi, tunatumia usihiri. Mambo yetu yanatawasiri mno, yao yanakwenda kombo. Sisi tunawaloga. Na sasa tuondokeje Korosho, mahali tulipoishi kwa vizazi vingi? ...Nyumba zetu zinateketezwa na Wakorosho ilhali askari wa polisi wanatazama tu, bunduki mkononi, hauwapigi mshipa. Wanawake na mabinti zetu wanabakwa dhahiri shahiri na polisi wanavifumbia macho vitendo hivyo. ...Tunauliwa tuputupu.(uk. 75).*

Tom Mangala aliwalipa polisi hela nyingi kuwapa ulinzi, kinaya ni kuwa Sajini na wavamizi wake bado walimvamia Tom baada ya Tom kumaliza shughuli za kumzika mzee wake. Walimwacha chini ya mwembe ajifie hapo. Akida anatueleza yaliyojiri waliporejea kutoka kudadisi hali ya kwao na polisi mmoja na sasa walikuwa wameingia garini tayari kuondoka ilhali Tom hakuwa ndani:

> *Hapo sasa ndipo alipokuwa kalala tani Tom, mikono kaitupa ovyo, shingo ameipinda... "Kuweni na imani bwana, mtu amewakodi kumlinda aje amzike babake. Anashambuliwa mnatazama tu, hamfanyi lolote. Askari nao wanaonyesha wamekandamizwa na mifumo. "Eeh! Ungefanya nini na wavamizi wanakuja wakiongozwa na boss wako mwenyewe? Kisha anakuamuru uwaachie wafanye watakavyo."(uk. 103).*

Katika Jarida alilopewa na Jerumani, Madodo alifahamikiwa na ukweli kuwa serikali ilihusika na vita vya kikabila na ili kujizatiti na mfumo huo wa ukandamizaji. Baaadaye Mbunge Johnstone Mabende alikabidhiwa Waziri wa Usalama wa Ndani. Jarida lilieleza:

*Mbunge Johnstone Mabende, wakereketwa wake na viongozi wa kidini Wakorosho na wasiokuwa Wakorosho walikuwa watuhumiwa wakubwa katika mauaji ya halaiki. ...Serikali iliyafumbia macho mauaji hayo kwa vile maafisa wa ngazi za juu serikalini walihusika. Vita hivyo vilikuwa kwa maslahi yao. Wakanju wakionwa kama wapinzani kwa serikali na kwa hiyo dhiki yao ilikuwa stahili yao. Imebainika wazi kuwa mheshimiwa Mabende alitaka kuwatimua Wakanju kutoka Wilayani Korosho kwa madai kuwa hawakumpigia kura katika uchaguzi mkuu uliopita (uk. 160).*

Ndi- anaeleza aliyoyaona katika TV yake alipoigungulia. Aliona masanamu ya robiti yaliyokuwa yakitekeleza maangamizi na fujo za kila siku. Maovu yalitekelezwa na polisi na raia walipata hasara kubwa. Maovu kama mauaji, nyumba kuchomwa na ubakaji yaliendelezwa na serikali – 'polisi'. Ndi- anasimulia:

*Walikuwa katikati ya zahama na kasi na fujo na mahana na utashi wa kupiga na kuhujumu na kufyeka na kuua. Magwanda waliyovaa yalielekea kama ya askari polisi au wanajeshi. Wengine wana mirau na wengine mapanga mikononi. Ghasia nyingi zilienea walipowatimua raia majumbani mwao na kuwafukuza kwa hujuma za kikatili. Walikimbia na kufukuza raia ambao kama wendawazimu wakipiga mayowe ya malalamiko ya maumivu ya kivita. Pigapiga, fyekafyeka, mateke ya mabuti. Zaidi walipita kumwaga risasi za mpatampataye, ovyo na kwa dhamira ya kuua. Na wale waliokuwa na mapanga wakichinyanga watu miguu na mikono; wake kwa waume walifyekwa, ingawa wanawake ndio waliosakama zaidi na wengine wakiwaangusha chini kuwainamia. Wazee pia. Hirimu, vijana na hata watoto wachanga. Wengine miongoni mwao walikuwa wanatia moto nyumba za watu. (uk. 159-160).*

Ridhaa anaeleza yaliyojiri kabla ya wao kujipata wamekuwa wakimbizi wa ndani kwa ndani katika Msitu wa heri. Mtafaruku baina ya sehemu hizi mbili za kisiasa zilizua hali tete na kilichozalika ni vita. Polisi waliwakandamiza raia na kusababisha hasara bila kujali. Ridhaa anatueleza:

*Hali ya taharuki ilitamalaki, vyombo vya dola vikatumwa kudumisha usalama katika vijiji, mitaa ikajaa sismizi walioshika bunduki. Hali hii ilileta chachawizo zaidi katika vijiji na mitaa. Binadamu ana hulka ya kushangaza! Hapendi kudhibitiwa. Kule kuwapo kwa walinda usalama kulimshinikiza binadamu kuhalifu sheria, ...Viongozi wenyewe baada ya kupiga kurea, walijikalia majumbani mwao, na kuendelea kutazama masabaha wao kwenye runinga wakiendelea kuzozana! Mchezo wapolisi kukimbizana na raia ulianza. Katika mchezo huo mamia ya roho zisizo na hatia zilisalimu amri chini ya pambaja za risasi na mapigo ya rungu, vitoza machozi navyo vikafanya kazi barabara. ...wakapoteza kila kitu, si maisha, si mifugo, si aila. (uk. 19-20).*

### 4.1.2 Upotevu wa Uhuru wa Kibinafsi

Uhuru wa kibinafsi unadhoofishwa na kuondolewa kabisa, huku watu wakilazimishwa kuishi kwa mujibu wa sheria na kanuni kali. Wahusika wanakabiliana na kutokuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yao wenyewe au kuwa na maisha ya kujitegemea. Udhalimu na udhalilishaji husheheni ukatili na mateso kwa binadamu ili kudumisha mfumo uliopo.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, mwandishi anatusimulia jinsi mwanamume mmoja alivyopoteza uhuru wake binafsi. Mkewe anamripoti kwa wachuuzi wenzake, akina Pam wanasimuliwa na mwanamke mmoja:

*Huyu bwana tukibeba naye mizigo pale soko Mjinga kwa miaka ngariba. Ni Mchungwachungwa huyu jamani na tohara ni jambo la lazima kwa wanaume wote miongoni mwetu sisi Wachungwachungwa. Basi mwanamke mmoja waliyezaa naye watoto wawili lakini hawajaoana, ndiye aliyemsaliti kwetu. Sisi kumkagua leo, Lo! Kumbe mwenzetu bado 'mtoto' ati. Basi tukaazimia tulifunge soko ili tuigotoe shughuli hii ya dharura kwanza. Wacha mtoto afanywe 'mwanamume' ndipo awe na akili. (uk. 55).*

Ujio wa Tamari, Tamari kumfokea Akida kuwa yeye ni Mkanju na kufutwa kwa kazi kwa Tim maana aliienda sherehe ya Akida ni mambo yaliyomsonga Akida asubuhi moja. Akida akatoka na kuzurura Jijini Tandika. Mawazoni mambo mengi yalimpitikia akilini. Hana wa kuelezea ila kujiamulia lililo bora:

*Je, babangu hajambo? Je, mitawahi kumwona tena? ...Je, ninao mustakabali wowote? Nitawahi kwenda Shule ya Kitaifa ya Upili ya Kiwachema nilikopewa nafasi? Nitasoma niwe msanifu ujenzi maarufu nchini? Au matamanio yangu yameyeyushwa na kutokomezwa na vita vilivyozuka kwetu kijijini. Nipande ghorofa nijitupe kama Mzee Yusuf Matuko? Au nijitupe mbele ya gari liendalo kasi? Nilale reli nisagwesagwe na treni? (uk. 65).*

Akida anaeleza jinsi walivyopoteza uhuru wa kibinafsi kutokana na wavulana kupashwa tohara na kwa bahati mbaya kuukata mpini wa mvulana na wakati mwingine wahusika kufa. Akida anasimulia:

> *Msimu wa ukeketaji wa kisu cha ngariba ukaja. Asubuhi moja nilishuhudia ngariba mmoja chongo akimtahirisha mvulana mmoja karibu na kituo cha biashara cha Binge. Alimkata mpini ukaanguka. Umati ukaanza kumpiga kitutu ngariba. Ni baadaye tu ndipo kijana majeruhi alipopelekwa hospitalini Sangura mjini. (uk. 172).*

Mtima alihitajika kuwa mwepesi kutekeleza masharti ya wakala wake aliyekuwa amemlipa dola elfu nne. Malipo hayo yalikuwa kama mshahara wa njama fulani. Pindi tu walipotua Uingereza, Mtima alifululiza hadi msalani kutimiza sharti kuu. Alichukua pasipoti yake, akaichana na kupiga maji flashi. Pindi tu mlango wa msalani unagongwa kwa kishindo. Hata hivyo alifaulu kupiga flashi na kipande cha pasipoti kilichokuwa kimeanguka chini akakitia kinywani na kukitafuna na kukimeza (uk. 80). Iwapo Mtima hangekuwa mwepesi kutimiza ujanja wa wakala angekamatwa na labda arejeshwe kwao nyumbani Kijiweni. Matokeo ya kupiga flashi pasipoti ni kuweza kuishi kule na ikiwezekana ajisajili kama mkimbizi. Mtima anapoteza uhuru wake na sasa atategemea ufadhili wa Waingereza.

Ndi- anamsimulia Naima, kivuli chake athari ya walowezi kwao Kijiweni. Wazaliwa wa Kijiweni wakapoteza uhuru wao. Ndi anaeleza:

> *Wengine walikuja waziwazi kwa nguvu za kutawala. Na kutawala maana yake kuwadunga watu sindano za nguvu za mafarakano. Chuki baina ya huyu na huyu zimejaa katika damu za watu mpaka leo. ...Ubaya ni kuwa wao ni wao tu, wao ndio bora kuliko watu wengine. Wao bora peke yao. Wao ndio wenye haki kuliko waliokuwepo hapa mwanzo kwa maelfu ya miaka. (uk. 98).*

Kivuli chake Yungi kipo pale mlangoni, dhahiri shahiri ametekwa na dawa za kulevya sasa yeye ni mraibu. Ilikuwa kama anahitaji hewa apoe, na ule moshi wa sigareti aliyokuw akivuta utoke nje (uk. 103). Anaendelea kumweleza baba mzazi kuwa "Najua kwamba mimi si lolote si chochote katika ukoo huu." ... "Nimeshakuwa mhuni, maluuni. Nakuaibisha baba!" (uk. 104). Mwenyewe anajishataki na kuona jinsi amekuwa mraibu wa raha ambayo ni karaha.

Ndi- 'anapopoteza uhai wake' kwake nyumbani kunafika wageni wa aina mbalimbali. Mmoja wao akiwa Mzungu wanayestarehe na bintiye Yungi anayetusimulia jinsi mabara mengine yametutawala hadi tukaupoteza uhuru wetu sisi Waswahili:

> *..."Sisi ndio tuliopewa haki ya kuudhibiti ulimwengu,"nikawahi kumsikia Mzungu mmoja aliyekuwa akibwabwaja kwa jeuri alipokwishaikata chupa ya Gorbachev. Alikuwa akimtumbuiza binti yangu Yungi aliyekuwa kaegesha kichwa mabegani pake. "Tulipoona haitoshi Ulaya na mabara ya Mungu matupu duniani; na watu wasiofahamu faida ya ardhi kama nyinyi mmeikalia kivivu, tulikuja kuing'wapura!" ...Ndiyo..Ndiyo..." aliendelea yule Mzungu. "Akili zetu ndizo zilizotupa haki tutawale. Nguvu na ubora wetu wa kimaumbile ndio uliotuwezesha kujitawaza. (uk. 126).*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatuelezea hali iliyowakumba mhusika Kairu. Baada ya machafuko ya kisiasa, Kairu na familia yake wakiwa mama na wanuna wenzake wanasombwa hadi kambini. Wakiwa na matarajio kuwa hali ingetengenea warudi makwao. Hata hivyo mambo yalikuwa tofauti. Ukimbizi unawapa hali ya kujiamini na kuukumbatia kisa na maana hawana matumaini ya kurejea kwao tena. Anasimulia:

> *Hata hivyo, tulijipa kuamini kwamba haya ndiyo yaliyokuwa majaliwa yetu, tulikuwa wenye haja, maiti hasa, na tangu hapo maiti hachagui sanda wala jeneza. Tulivumilia, tukawa tunaishi kwa tumaini tukidhani hali itatengenea, tukitumaini kwamba tungerudi kwetu. Lakini lo! Wanasema kuwa msitu ni mpya, ila nyani ni wale wale. Uongozi mpya haukuleta ahueni yoyote katika maisha yetu! Kilichobadilika ni kwamba tulipewa ardhi zaidi ya kujenga mabanda zaidi ili kupunguza msongamano katika mabanda ya awali. Bado tu pale pale. Nilikwenda hapo nikiwa darasa la sita. Sasa ni kidato cha pili. Tungali tunasubiri kurudishwa nyumbani! Ila sioni kama pana nyumbani pema zaidi ya pale kambini ambamo tunaishi bila kujali tulipotoka. (uk. 92).*

### 4.1.3 Teknolojia na Utandawazi

Mohammed na King'ei (2008) wanaeleza utandawazi kuwa ni dude linalopita na kuathiri maisha ya wanajamii katika sekta zote za maisha yao. Kupitia utandawazi, tamaduni na fasihi za magharibi zimepokezwa waafrika. Hali hii hudhihirika katika fasihi andishi ambazo ni zao kutoka magharibi, maudhui namna waandishi wanavyosawiri wahusika wao. Khamis (22008) anasema kuwa nchi changa zimekuwa nchi pokezi za utamaduni wa wageni hasa zile mbaya. Nchi changa katika muktadha huu zinapatikana katika ulimwengu wa tatu ambapo mandhari za riwaya zinazohakikiwa katika tasnifu hii.

Kulingana na Wanjiku (2018), utandawazi umechangia mabadiliko katika sekta mbalimbali za jamii kama vile desturi, mila, heshima, dini na utamaduni. Alsaedy (2015) anasema kuwa kutokana na utandawazi, kumekuwa na mivutano kati ya watoto na wazazi, jamii na jamii katika Bara la Afrika. Watoto wanaiga tabia kutoka magharibi na kuona kama tamaduni za Kiafrika zimepitwa na wakati. Wazazi wa Kiafrika wamejipata katika njia ya mtanziko kwa sababu ya mabadiliko yanayoathiri tamaduni na amali za jamii zao asilia.

Utandawazi na teknolojia hutumika kama chombo cha udhibiti na ufuatiliaji wa watu. Kamera za ufuatiliaji, kamera za usimamizi, intaneti, kompyuta za kisasa na akili bandia mara nyingi huonekana zikidhibiti maisha ya watu, kupunguza faragha na kuendeleza udhalimu. Vifaa hivi hufuatilia watu na mienendo yao na kuweka idhibati ya kurejelea.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* Akida anaposafiri kwenda jijini Tandika kwa shughuli za kuzawadiwa anakuwa mwenyeji wa Tim. Tim alifanikiwa kununua televisheni kuwapasha habari na jioni moja Tim anamfunza Akida jinsi ya kuiwasha. Katika habari za televisheni wanatangaziwa habari kuwa vita vimefumuka kwao Baraki kijijini:

> *"Waziri wa Usalama wa ndani mheshimiwa Panga Lutulia, amekanusha habari zilizochapishwa na baadhi ya magazeti ya humu nchini kwamba vita vya kikabila vimefumuka katika eneo la Baraki, Wilaya ya Korosho. Waziri alisema habari hizo hazina msingi wowote bali ni uongo wenye nia ya kuchochea uhasama kati ya makabila yanayoishi sehemu hiyo. Aliwashutumu waandishi wa habari hizo ...Matoleo ya leo ya baadhi ya magazeti yalikuwa yamedai watu kadhaa wamekufa, wengine wengi wamejeruhiwa na nyumba nyingi zimeteketezwa, baada ya vita vya kikabila kufumuka baina ya Wakorosho na Wakanju Wilayani Korosho (uk. 28).*

Teknolojia imetumika kupasha habari na zaidi kueneza uvumi ili kuchochea vita vya makabila. Ingawa waziri anajaribu kukataa kuwa huo ulikuwa uvumi, matoleo zaidi yalisema kuwa vifo vya kikabila vimeripotiwa Baraki. Tujuavyo Baraki ndipo kijijini walipotoka Tim na Akida. Kule kijijini ndipo Bwana Sululu alipobaki akiugua na baba yake Tim.

Tim alimweleza Akida kuhusu habari za kwao Baraki. Alikuwa amepigiwa simu na Tom, mtoto wa pekee wa Mzee Mangala kuwa Baraki kumechacha vita. Kifaa cha teknolojia ambacho ni simu kilikuwa kimewapa habari za kutamausha kuhusu kwao. Mwandishi anatutongolea:

> *"Tom amenipigia simu kazini," alisema Tim.*
>
> *... "Ulisema kakupigia simu?"*
>
> *"Ndiyo. Amenipigia simu akasema nyumbani ni kubaya. Baraki hakwendeki Akida." (uk.58-59)*

Mwandishi anatuelezea jinsi mashine na vifaa vingine vya kiteknolojia vinavyoozeana pale Hospitali ya Rufaa ya Tandika. Akida anatueleza:

> *Tulipita uwanja mmoja baina ya majengo, uliosheheni mashine kadhaa zilizolala ovyoovyo – zimevunjika, zimeharibika, zimeota kutu – hazitamaniki (uk. 72).*

Hali ya vifaa ni ya kuhuzunisha katika hospitali kuu ya kiwango cha rufaa. Vifaa ambavyo vinafaa kuwasaidia wagonjwa ilhali vimevunjika. Tunamwona hata mgonjwa mmoja akijifia kwa machela bila kuhudumuwa na daktari au vifaa hivyo.

Mwandishi anatuelezea kuwa baada ya Tom kusoma na kuhitimu kutoka Marekani, alirejea kijijini na kumnunulia baba yake Mzee Mangala runinga.

> *Tom alipomnunulia babake televisheni ndipo nilipolimbuka kuona kioja kile cha kiteknilojia. Umati wa wanakijiji ulifurika furi kwa Mzee Mangala na kukiajabia kidude hicho (uk. 80).*

Televisheni hii iliwaonyesha mambo mengi hasa kandanda kwa vijana.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Yungi anawaeleza wazaziwe kuwa enzi hizi za utandawazi mambo yamebadilika. Usemi wake unaakisi athari ya utandawazi unaochangia mmomonyoko wa maadili – kijana huyu Yungi anaposema haya yu mlevi:

> *Wakati wanaume. umebadilika. Watoto kuanzia sasa watawaendesha wazee wao. Pia huu ni wakati wa wanawake kuwakimu na kuwaongoza wanaume... (uk. 25).*

Mwandishi anatuelezea mtagusano wa Ndi- na Bi. Muse. Mazungumzo yao yanazua bustani tofauti zilizo na maelezo linganifu ya maisha. Maisha kama mmea Ndi- aliougusa yalinawiri, alipokidondoa kidole chake mmea ukanyea. Bustani nyingine aliona majengo marefu – *ki-Villa,* iliyojengwa na wafisadi. Bustani nyingine alikuta kila kitu kimepandwa na kuundwa ki-*hybridbybrid.* Walipoendelea kutarazaki na Bi. Muse wakaingia bustani ingine iliyojaa *cloning*. Bi. Muse alimfunulia makuu ya teknolojia na hayo yalifanikiwa kwa kuwepo kwa kompyuta aliyomtumia Mtima.

Ndi- anatuelezea uchakaramu wa mwanaye Bori wa kuokota vitu hasa vya stima yote katika harakati za kuendeleza utandawazi. Tarajio la Bori lilikuwa familia wamwone kama mhandisi mashuhuri lakini wakati mmoja moto karibu uwaangamize.

> *"Wakikushinda kwa huu, washinde kwa ule. Nitakuwa mhandisi." Unyamavu wa Bori urokotea wake wa vyombo vya stima, utundu wake wa vyombo vya umeme ...ilikuwa pia namna yake na uyeye. (uk. 112).*

Mwanawe Bori aliyekuwa amefeli mtihani wake alikuwa anathibitisha msemo wa kisasa kuwa "soma ujitegemee' ndiposa alijitwika jukumu la kuokota vyombo na kuuza vilivyo vya maana.

Ndi- anapofungulia TV yake aliona mambo yaleyale aliyokuwa akiyahofia ya maangamizo ya kila siku.

> *...Walikuwa kama masanamu ya roboti yaliyokuwa yakiendeshwa na remote control na gangster mkuu pahala fulani pa siri. (uk. 159).*

Teknolojia nayo ni kigezo cha kuendeleza maovu ya kijamii kwa kuyaweka wazi na labda kuhimiza akili kulenga fujo.

Wakaazi wa Msitu wa Mamba – wakimbizi akina Kangata, Ridhaa na Selume, waligunduliwa kuwa walikuwa wakiishi pale kiharamu. Viongozi wakapanga njama ya kuwafurusha. Mwandishi anatusimulia:

> *Vyombo vya habari havikukawia kutoa wito wa chama tawala kuwatafutia watu hawa mahali kwingine, vidonda vya zamani vikaanza kutoja damu. (uk. 75).*

### 4.1.4 Ukosefu wa Usawa na Unyonyaji wa Kijamii

Jamii za distopia mara nyingi zimegawanyika kati ya matajiri na maskini, wenye nguvu na wanyonge. Matabaka huzuka na kuwapa wenye tabaka moja nguvu zaidi za kudhibiti tabaka lingine. Wanaodhibitiwa huwa wengi na ndio huishi katika hali ya unyonyaji, wakati wachache wanapata faida kutoka kwa mfumo wa udhalimu. Tabaka la wasionalo huitwa maskini kwa kukosa mahitaji ya kimsingi kama maji, chakula, makazi na hata usalama. Umaskini ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya jamii. Vijana wamo mbioni kupambana na uovu katika jamii na kuleta mabadiliko.

Katika *Kufa Kuzikana,* Akida anamulika uovu unaoendelezwa na wafanyakazi wa umma hata katika sekta ya elimu. Mwanafunzi aliyeibuka nambari moja; Regina Kato alikuwa mpwa wa Waziri wa Elimu. Naye Donald Kitenge aliyeibuka nambari mbili alikuwa mtoto wa mfanyakazi wa ngazi za juu katika Baraza la Mtihani wa Taifa (BMT). Akida anasema:

> *Nilishindwa kujizuia kutuhumu sakata ya namna fulani katika mchakato mzima wa mitihani ya taifa. (uk. 51).*

Akida anaonyesha wazi jinsi ukosefu wa usawa unawakosesha nafasi sawa katika viwango vya elimu. Kijana huyu anshutumu wachapishaji kwa kukawia na miswada ya watu kwa sababu wandishi wengine hufa hata kabla ya kuiona kazi yao imeandikwa. Anasema:

> *Mgonjwa ndio namna amenituma kwako, Ataka ajue diwani yake itachapishwa lini? Mbona nyie wachapishaji mnakawia sana na miswada ya watu? Kama mswada ni mbaya hauchapishiki rejeshea mwenyewe haraka. (uk. 51).*

Tamari, dada yake Tim aliwaeleza kina Pam na Tim yaliyojiri kwao Baraki. Pam anamsimulia Akida aliporejea kwa nyumba yake Tim pale Shauri Moyo:

> *Walijaribu kumnajisi akajinasua na kuwakwepa. Ametembea kwa miguu na kulala msituni siku kadhaa. Ameona maiti ngapi pale alipo. Anasema alipata lifti kwa lori ya wafadhili wengine waliomleta mpaka hapa kwenye geti..." (uk. 68).*

Anayoyasimulia Tamari ni wazi kuwa jamii hiyo inakosa usawa wa kutetea haki. Hata wakati wa vita wanaume lengo lao ni ubakaji na kuhujumu haki za wanawake. Mauaji ya kiholelaholela pia yanaonyesha jamii iliyokosa mustakabali wa amani.

Zaidi, jamii imekumbwa na umaskini na matabaka ya walalahai na walalahoi yamebainika wazi. Tim alipopigwa kalamu alikokuwa akifanya kibarua, alienda kuishi katika mtaa wa Falkland ambapo kijana huyu aliishi na dada yake Tamari na rafiki yake Akida. Tunafahamishwa mandhari ya mtaa huo ambapo yanadhihirisha umaskini wa hali ya juu. Tunasimuliwa hivi:

*Mtaa wa Falkland, maarufu kwa jina la Kambichafu ulikaa akina pangu pakafu. Mabanda yaliyopachanapachana yenye kuta zilizokandikwa udongo na kuezekwa mabati yenye vishimo na kutu ndiyo yaliyoitwa nyumba. Tope lilijaa kwenye vijia vilivyokuwa baina ya mabanda hayo yaliyoinamiana. Fondogoo ya marundo ya taka zilizotoa maji ya mvua na mikojo ya watu, ilichangamana na harufu ya vinyesi vya watoto na watu wazima vikaunda mseto na mnuko mbaya sana. (uk. 110).*

Akida alikuwa bado na hamu ya kusoma. Ahadi aliyompa Tom walipomaliza kumzika Mzee Mangala aliona haingetimia maana Jenelle alikuwa amehamia Canada na kurejea na kumchukua mumewe apate matibabu na waishi kule. Akida aliwazia ahadi alizopewa na Waziri wa elimu kuwa wangegharamia masomo yake lakini kwa bahati mbaya alikuja kugundua njama fiche. Njama ambayo ilimkosesha ufadhili na nafsi ya kuendelea kusoma. Akida anasema:

*Baada ya 'nenda urudi kesho' nyingi, nikaja kugundua kuwa nafasi yangu katika Shule ya Kitaifa Kiwachema, nilikoitwa, ilikuwa imetwaliwa na mtoto wa tajiri mmoja. Aidha udhamini wangu kutoka kwa wizara, ulikuwa umepotea. "Umechelewa,"aliniambia sekretari mmojawapo katika ofisi za wizara. "Umechelewachelewa ukakuta mwana si wako." ..."Waziri hawezi kuonana na mtu uchwara kama wewe," nilizuiwa na sekretari. (uk. 126-127).*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* wanafunzi wanaopata nafasi ya kuenda na kuendeleza maisha yao ughaibuni wanakumbana na hali tata inayowaweka mawazo na kudhihirisha ukosefu wa usawa wa binadamu. Mtima katika barua yake kwa baba yake Ndi- anasimulia hali ngumu anayoipitia:

*Nimo tu mpaka sasa nagaragara kwa wenzangu ambao kwa muda mfupi wameshanichoka. Sina budi lakini kung'ang'ania. Ndivyo maisha ya hapa yalivyo. Kila mtu hubeba mzigo wake. Kila mtu hujitakia mwenyewe, hamtaki mwingine. Ikizidi dakika moja ya kuwekwa na mtu nyumbani kwake, basi balaa. Unaikumbuka ile nyimbo tuliyoimba shulen? "Mgeni siku ya kwanza mpe mchele na panza...Mgeni siku ya kumi kwa mateke na magumi..."(uk. 7).*

Ndi- anaelezea kisa alichohudhuria na kutoa nguo na kubaki nusu uchi. Alipiga ukwenzi na kusimama juu ya meza kuhutubia waliohudhuria sherehe hiyo. Anatuonyesha jinsi hata iwapo wako kwenye hafla moja, hawana usawa na kuna unyonyaji. Ndi- anahutubia:

*"Hakuna udugu, kuna uhasama wa mtu na mtu!" Nilipiga kelele huku nikiashiria kidole kwa kila mtu. "...Hakuna sisi katika dunia hii!" Nilionyesha ishara ya ile tafrija nzima. "Kuna mimi!"Nilijionyeshea kidole. "Kila kitu ni mimi, na mimi, na mimi ...Hakuna usafi wa sote ila uchafu wa mtu binafsi. Mnakula nini? Hamwoni? Hamjui kwamba mnakula mizoga? Hamjagundua kwamba mnafakamia mafunza na matapishi? Ishara ziwe zipi zaidi kuliko hizi?" (uk. 84).*

Matokeo ya hiyo hotuba ni alitekwa mzimamzima kama kitakataka akavalishwa nguo na kupelekwa polisi. Waliomkamata ni wale aliokuwa akiwatetea. Aliwekwa rumande mpaka uamuzi fulani ufanywe. Baadaye aliwekwa gerezani na kule kazi ya sulubu ikamchosha. Analolikumbuka ni kuwa alichukuliwa hospitalini. Pale hospitali hawakuwa na vyombo vya kupima uwendawazimu. Ndi- aliwavamia mhudumu ikabidi aandikiwe ripoti na daktari waliyefahamiana naye vizuri iliyomfanya aachiliwe huru.

Mataifa yanayoendelea kwa msingi wa uhitaji au ulitima uliokithiri. Bara la Afrika linaonyeshwa kama lililogubikwa katika umaskini uliokithiri. Hali ya uhitaji inazua hali ya utumwa na kunyonywa nguvu na walala hai. Mwandishi anaeleza kuwa:

*Unaambiwa huruhusiwi kufanya kazi na sheria ya kutoruhusu ipo. Lakini hapana asiyejua kuwa kila mgeni hapa huja kutafuta kazi. Kila mtu ana maslahi yake-hatima na baadaye yake. Na jambo hilo maana yake ni kufanya kazi. Tena za nguvu naa kuumuka kama mtumwa. Malipo mkia wa mbuzi. Huna bima, huna kitu chochote cha kukulinda. Shauri yako, si umetaka kuingia peponi? ...leo tunajiuza wenyewe kwa hiyari zetu. (uk. 119-120).*

Kupata na kukosa sio rai kwamba uzuri na ubaya unakuja kutoka urithi tuliokuja nao duniani. Ni asasa mbalimbali au serikali mbalimbali zinazotusababishia matabaka mawili makuu:maskini na tajiri. Ndi- anatueleza:

*Kwamba umma mkubwa zaidi umejikuta tu ndani ya tanuri la mateso na wachache ndani ya kasri la tafrija. (uk. 172).*

Ndi- anasema na kivuli cha Shaaban Robert kinachosema:

> *"Nyinyi ni mfano mzuri wa kutaka kujiua kwa ajili ya wengine," alituambia, "ndio maana mnaitwa wakorofi na wale wakaidi wanaotaka kujenga nyumba bila ya kubarikiwa au wanaokusanya mali kwa nafsi zao na jamaa zao tu. Dunia yetu sisi haikuwa hivi. Yenu, isiwe wala haiwezi kuwa kama yetu, lakini mmewacha mengi mazuri tuliyokurithisheni. Mtaangamia!" (uk. 193).*

Baadhi ya wanajamii wanawanyonya wanajamii wenzao. Shaaban alikuwa akisisitiza ukosefu wa usawa upo na unaendelea kunawiri.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatuelezea taarifa ya habari kutoka runinga ambayo Ridhaa anakumbuka. Ridhaa anakumbuka jinsi alivyotazama majumba yake matatu yalivyobomolewa, kisa na maana ni mlowezi Msitu wa Heri – yeye si mzawa pale. Hili ni dhihirisho la unyonyaji wa kijamii kwa mirengo ya asili na kuonyesha wazi ukosefu wa usawa baina ya binadaamu (uk. 13).

Ridhaa anatuelezea yaliyojiri kabla wajipate wakimbizi Msitu wa Heri. Jamii hii ilikosa usawa wa kijinsia na kumdhalilisha mwanamke. Jamii hii haikuamini kwamba mwanamke anaweza kuwa kiongozi. Pindi tu mwanamke alipochaguliwa kulizuka rabsha na vita vikachacha. Ridhaa anatueleza:

> *Siku ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya, kiongozi ambaye kulingana na desturi za humu mwetu hakustahili kuiongoza jamii ya Wahafidhina, kisa na maana, alikuwa mwanamke, mbingu zilishuka. Watu walishika silaha kupigania uhuru wao; ambao walidai hawakupewa, walijinyakulia kwa viganja vyao. Tetei, mwanaharakati mmoja, alisikika akisema, "Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike- ...enzi ya kiistiimari wanaume walivyotumikishwa! ...Kwa miongo mitatu sasa, hawa watu wamekuwa wakitusumbua na Affirmative Action, na A third should be women (uk. 17).*

Mwandishi anatuchorea picha ya hali halisi ya mataifa mengi ya Bara la Afrika yaliyo na rasilimali nyingi kama maji, mawe ya ujenzi, vito na mafuta lakini yamenyonywa na kuachwa maskini hohehahe. Wageni wanawaajiri wenyeji kazi za kijungu jiko. Mazungumzo kati ya Tila na babake Ridhaa yanaweka wazi ukosefu wa usawa na unyonyaji. Mwandishi anasema:

> *Tila:...Lakini tayaru kuna kampuni za kibinafsi ambazo zimetumwa huko kuchimbua madini haya. Isitoshe, kampuni zilizoshinda zabuni za kuyachimbua madini haya ni za kigeni. Uchimbaji wenyewe unafadhiliwa na wawekezaji wa kigeni. Raia watafaidika vipi? Fedha zinazotokana na rasilimali hii yahofiwa kuwa zitaishia kwenye mifuko ya wageni. Zinatumiwa kuendeleza nchi zao na hao hao wawekezaji wanaodaiwa kuwa wahisani. ...Ridhaa: Ni kweli, lakini kumbuka kampuni hizi zimebuni nafasi za kazi. Wenyeji wamepata ajira Tila: ...Ambayo mshahara wake ni mkia wa mbuzi. ...(uk. 44)*

Mwandishi anatusimulia kisa cha mwanawe Kiriri, Lunga kwenda hospitali kutibiwa baada ya kukeng'etwa na homa ya matumbo. Mwanafunzi mwenzake Kimondo anaigiza jinsi daktari mwafrika alivyombagua kwa sababu baba yake ni kibarua:

> *"Daktari, Mwafrika mwenzako, anakukazia macho na kumwambia muuguzi, 'His father is a casual labourer. We cannot treat him. The company does not have any medical scheme for casual labourers.' Muuguzi anayasikiliza maneno haya, na baadaye kuwa mkalimani wako, anadhani huelewi lugha hii. Sijui Lunga kama umewahi kujiuliza kama huduma bora za afya zinastahili tu kwa watoto walio nacho. Je, mwana wa kibarua, ambaye ndiye anayezalisha mali ya kuwezesha kuwepo kwa hiyo medical scheme hastahili kupewa huduma hiyo ya matibabu? ...(uk. 70).*

Mwandishi anatudondolea mambo yanayoonyesha jamii iliyokosa usawa na inayonyonya wasomi wake kupitia mhusika Shamsi. Shamsi ni jirani wa Ridhaa, anaishi mtaa wa Kazikeni uliomkabala na wa Afueni ambapo Ridhaa anaishi – makazi mapya ya Mwangeka. Shamsi ni msomi aliyekuwa wa kwanza kijijini kufuzu ilhali kaambulia vibarua kwenye kampuni ambapo analipwa mshahara mdogo ambao anautumia kunywa pombe tu. Shamsi anatuelezea hapo kuwa iwapo ulihitaji kazi nzuri lazima utoe hongo. Mwandishi anatusimulia hali ya Shamsi kupitia ngonjera anayoiimba akielekea makazi yake duni:

> Kwani hawakunikabidhi kazi
>
> walizoahidi kwenye mabuku?

Kwani hawakunipa nyenzo

za kujiendeshea maisha?

Kwani walitupuuzilia mbali

tulipolilia kuhiniwa?

Nafasi za kazi

tulipotwaliwa

Na ndugu zao

huku tukiambiwa kindanindani

'Viganja huoshana,

aso mwana aeleke jiwe!'(uk. 132-133)

### 4.1.5 Kukosa Maadili na Kuanguka kwa Maadili ya Kijamii

Maadili ya kijamii yanadhoofika au kuanguka kabisa. Hali hii hupelekea kupotea kwa utu na hisia za kibinadamu. Kuna mambo kadha wa kadha yanayoashiria mmomonyoko wa maadili kama vile ukosefu wa huruma, haki na utu ambapo watu wanafanya vitendo vya kikatili bila kujali madhara kwa wengine. Maadili yanapotoka katika jamii yenye utawala wa kimabavu na hali tata kama vita na maovu mengine husheheni.

Enzi hizi wanajamii wengi hujihusisha katika mapenzi na ngono za kiholelaholela na kuliona jambo hilo kama la kawaida. Hasa vijana, hupoteza mwelekeo kwa kuishi bila kuzingatia mwongozo mwema katika shughuli zao za maadili. Fursa na uwezo wa kuishi maisha bora hupotea kaw sababu ya athari ya mapenzi ya kiholela.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana*, Akida, Pama na Tim wanapotoka sherehe ya kuzawadiwa kwa Akida, wanaliabiri gari moja na kumbe ndani limejaa. Tim akampa abiria mmoja zawadi ampakatie. Bahati mbaya waliposhuka wakaisahau na huo ukawa ndio mwisho wa Akida kuiona zawadi yake. Abiria angekuwa mkarimu angeiacha kwa gari maana Tim walilingojea njiani liliporudi na wakalisimamisha. Mwandishi anatueleza yaliyojiri;

> *"Tumesahau kitu hapa," Tim alimwambia kondakta. Kondakta akatuambia hamna chochote pale ndani. ...Tulitafuta tusione chochote (uk. 57).*

Hili ni dhihirisho wazi kuwa abiria wengine wanakosa maadili na kushuka na mzigo wa wenyewe.

Tamari anamfedhehesha Akida kuwa hajapashwa tohara. "Kama mngekuwa mnaona kisu cha ngariba mngekuwa watu." Hii ni ishara wazi kuwa Akida na Wakanju wenzake hawakuwa wanatahiriwa. Lakini kusema haya ana kwa ana ilionekana ni wazi kuwa Tamari alikosa maadili ya kimsingi.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* Akida naye alikuwa mwanafunzi mwerevu sana shuleni na aliyapenda sana masomo yake. Katika mtihani wa taifa wa shule ya msingi, Akida alikuwa miongoni mwa watahiniwa watatu bora kote nchini Kiwachema. Alikuwa mmoja wa wale watatu bora waliozawadiwa na Waziri wa Elimu. Alipokuwa akihojiwa wakati wa kuzawadiwa, alisema kuwa alinuia kusoma sana hadi awe msanifu ujenzi na kuzuia ajali zinasosababishwa na majengo yaliyojengwa vibaya kwa sababu ya ufisadi. Alikuwa na ndoto nzuri sana ya kuleta mabadiliko katika jamii baada ya kuhitimu masomo yake lakini masomo yake yalikatizwa wakati wa vita vya kikabila vilipozuka nchini mwake. Walipopashwa habari za kuzuka kwa vita wakiwa jijini, Akida alishtuka sana na kujiuliza maswali kama haya?

> *Je, babangu hajambo? Je, nitawahi kumwona tena? Je ninao mustakabali wowote? Nitawahi kwenda shule ya kitaifa ya upili ya nafasi? Nitasoma niwe msanifu ujenzi maarufu nchini? Au matamanio yangu yameyeyushwa na kutokomezwa na vita vilivyozuka kwetu kijijini? (uk. 65)*

Akida alikuwa miongoni mwa walioenda Baraki kumpumzisha Mzee Mangala. Njiani hawakusimamishwa kwa sababu Tom alikuwa amekodi polisi kuwalinda safari yote ili wapumzishe mzee. Lakini msimulizi anatueleza kuwa wakati mwingine polisi uwasachi hata maiti kisa na maana ni kuwa; ...Kiwachema kuna baadhi ya walanguzi wa dawa za kulevya husingizia wamechukua maiti jenezani kumbe ni shehena za dawa hizo (uk. 92). Hili linaonyesha kuwa maadili yalikuwa yameporomoka hata kwa wafu. Hata hivyo hao

wahalifu walikwepa mkono mrefu wa serikali kwa kutoa hongo. Mwandishi anatueleza kuwa bora mkono uende kinywani (uk. 93), utaepuka kunaswa na dawa zako.

Akida alijihusisha kimapenzi na msichana aliyeitwa Susana, jambo lililomfanya Susana kuacha masomo yake na kuolewa. Akida anaeleza mambo yalivyomwendea mrama:

> *Nilimdondokea msichana mmoja rafiki ya Cynthia, jina lake Susana. Walikuwa wakisoma pamoja na kutembeleana sana. mambo yalianza kwa kukonyezana macho hadi tukajikuta tumetumbukia katika lindi la mapenzi na makosa mazito. Dhambi hasa. Nilijaribu kwa jino la ukucha kumficha Susana siri ya kutotahiriwa kwangu. Ila baada ya 'kitendo' nilikuwa nikihisi hatia hususan nilipokumbukia mahubiri ya Kasisi John Njalala Jijini Tandika. Nilishangaa mno Susana alipokatiza masomo na kuolewa na Joseph, mtoto wa mjane jirani wa mwajiri wangu. (uk. 169).*

Ni dhahiri shahiri kuwa huyu Susana kawa na wapenzi wawili aliojihusisha nao kingono, kisa na maana ni ghafla bin vuu aliolewa na Joseph na kumtelekeza Akida. Na lililo wazi ni kuwa Susana hakukamilisha masomo yake. Akida anasema:

> *Akaenda kwa Joseph mwana wa mjane na aliyekuwa mumewe Susana na rafiki yangu ya awali. Susana alikuwa kigoli aliyekatiza masomo kwenye darasa la tisa ili aonje tamu na chungu ya ndoa. Susana alikuwa mke mchanga, mbichi na mchafuchafu. Alipopewa barua kusoma alianza kutetemeka na kupenga kamasi ovyo ovyo. Alinitupia jicho mara moja kwa haya. (uk. 178).*

Akida alipoenda Kituo cha Polisi cha Kati Jijini kujisalimisha kwa kosa la mauaji, anakumbana na wengine walioshatakia kuvamiwa na wezi usiku, wengine kapigwa chupa na kadhalika. Alirushwa ndani ya seli kungojea hukumu yake. Ndani ya seli kulikuwepo wezi, wasinzi, wapiga kabari, wabakaji, walanguzi, waliotumia dawa za kulevya, wavutaji bangi na sigara na wendawazimu. Lililomshangaza kabisa ni kuwaona wanaume wanawakiana tamaa wao kwa wao na kutendana kinyume na maumbile, huku wamejitoa kimasomaso. Mle ndani alimkuta Kasisi John, kumbe aliwajua kimapenzi wasichana wanane ambao hawajafikisha umri wa miaka kumi na minane na alihukumiwa miaka ishirini, afanye kazi ngumu na kuchapwa viboko vinne. Baada ya uchunguzi ilibainika kuwa aliyemgonga mbao alikuwa Tembo na si Mzee Zablon. Mzee Zablon alijifia miezi minane iliyopita kwa kujitia kitanzi. Barua aliyoiandika kabla kujitia kitanzi ilizungumzia pia jinsi alivyomuua Mzee Sululu:

> *Kuuwawa kikatili kwa muke na wadodo wango wasio na hattia kumeniattua mooyo. Mie nimewauwa Wakanju wengi vittani. Nilikua mstari wa mbele katika kikosi cha Wakorosho. Ila sasa nashindwa kuhimili majutto ya kumuuwa Ndugu yangu Sululu, mutu asie hattia. Samaani Sululu.*
>
> *Zablon Mapisi.*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* mwandishi anatueleza maovu ya mwalimu wake ambayo wazi ni ukosefu wa maadili. Awali Ndi- alitaka kuiga mfano wake lakini baadaye mfano wake ukamuudhi. Ndi- anasimulia:

> *Sikudhani kama angeweza kulipaka jina lake kinyesi kwa kuuza haki za watu. ...Kilikuwa kikitoka duka fulani la Mhindi ambako watu walisema kikipokea mshahara mwingine zaidi kwa kusaidia kuendeleza na kudumisha mambo yawe mabaya kama yalivyo au zaidi. Kilikuwa kimojawapo cha vivuli vya watu vilivyopokea mishahara mingi kwa kazi chache zenye kuhatarisha maisha ya watu wengine. (uk. 30).*

Ndi- anashuhudia zogo la kundi la watu likimwongoza kibaka aliyekamatwa na kitoto kijanajike cha miaka minne. Damu zinamvuja. (uk. 31). Mwandishi anatumulikia uozo katika jamii ambapo watoto wadogo wako hatarini hata wa miaka michache, wanabakwa bila huruma.

Ndi- anatueleza kuwa alipofika Mkamasini, jizi lilikuwa limewachenga watu waliokuwa wakilifukuza. Lilikuwa limemvamia Sadiki Tumbo na kumkamatia bastola bandia ili atoe pesa na vyombo vya dhahabu. Sadiki alitoa. Jamii iliamini kuwa hela zile hawangezifanyia jambo la maana.

> *"Eeee, wanatafuta pesa za unga." (uk. 32).*

Pesa zile za haramu walizitumia kununulia madawa ya kulevya.
Kuporomoka kwa maadili kunadhihirika tena kwa kisa cha Kudemba. Ndi- anatueleza yaliyojiri katika kibanda kimoja:

*Mama alikuwa akibumburushana na mwanawe barubaru, kumlazimisha kulala kitanda kimoja naye. Kijana alipigana kujipapatua na dhambi hizo. Lo! Salaala! Lini Nabii Luti atafufuka kuja kuuokoa umma wa Sodom na Gomora? (uk. 34)*

Ndi- anatueleza kuwa alipogutuka kutoka ziara zake na Naima, alipata kuwa aliyemshika mkono alikuwa Bi. M. Ukumbini mwa nyumba yake Yungi alikuwa amefungwa bendeji kisa na maana Jitu nduguye alimgonga. Jitu amekosa maadili anatumia dawa za kulevya. Ndi- anatueleza:

*Kasimama ukumbini akiporoja na kucharaza kutukana matusi ya ajabu kuhusu ndugu yake jitu aliyempiga Yungi kigongo cha kichwa na kumpasua. Kisa? Yungi alilalamika kwamba Jitu ana mtindo wa kuuza vitu vya nyumba kununua unga. Alianza kuuza khanga na kanzu za Yungi, lakini jana aliuza redio na tepurekoda yake. Yungi alipolalamika Jitu alimpiga kigongo cha kichwa Yungi. Walipelekana polisi, lakini alikaa ndani saa moja tu Jitu. Watumiaunga wenzake waliununua uhuru wake polisi. (uk. 101).*

Mwandishi anatuelezea jinsi Waafrika wamekubali athari za kigeni na kushawishika kwa urahisi kuupokea utamaduni wa kimagahribi. Bara la Afrika linaiga kila kitu hadi mitindo na mavazi. Ndi- anasimulia:

*...mara tukashtukia tumeingia katika sherehe fulani...kwetu iliitwa fensi...'carnival' kwa lugha ya kisasa...(uk. 173).*

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) *carnival* (kanivali) ni sherehe ya kitamaduni ambapo waigizaji hijivisha mafigu yafichao sura zao na wakaigiza nyadhifa zisizokuwa zao. Mwandishi anatueleza jinsi maadili yanaporomoka kwa sababu katika maonyesho haya wengine waliwaiga warusi, waachina, na mienendo yao ya kikomunisti.

Ndi- anatusimulia kisa cha mwenzake Bwana Ndera kilichodhihirisha jinsi maadili yalivyoporomoka kwake:

*Utajiri wake, inasemekana, aliupata kwa kuteka ngawira kwa wale mahasimu zake aliowafyeka katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Siku hizi anabana kinyesi cha kuku kutafuna. ...vijana wake wawili waliishia jela ya wendawazimu kwa unga. Mmoja kafungwa jela kwa wizi. Na binti yake kafa kwa umeme. Kubwa zaidi, mkewe Masika, au kwa jina maarufu Kisura, kamkimbia. Kachupia farasi mwenye soji jema kwenda ng'ambu nyingine ya uchumi. (uk. 128-129).*

Mwandishi anatuelezea hali katika familia ya Ndi- ambayo ilipelekea Ndi- kukamatwa na hakimu alipoamrisha Ndi- kupimwa akili ikatokea kuwa ana wendawazimu, sheria ikamfunga na kuamuru abaki jela maishani. Jitu amembaka dada yake Kilua. Ndi- alisingiziwa na wendawazimu na kudhaniwa ndiye kaua Jitu ilhali Bi M alisema ni Yungi aliyemdunga Jitu kisu mara kadhaa akafa. Familia iliporomoka kwa kukosa maadili. Mwandishi anatuelezea jinsi maadili yalikosa zaidi kwa familia ya Ndi-:

*"Chumbani mwako ulikuwa unajitupa kitandani ndipo uliposikia ukwenzi na sauti ya uombezi ya Kilua. Hata hukujua vipi uliokota kisu juu ya meza. Ukakupuka. Mbio – ti, ti, ti. Moja kwa moja ukaelekea chumbani kwa Yungi. Mlangoni mkagongana vifua na Yungi Yeye aliwahi kuingia mwanzo chumbani na wewe kama wimbi ukafuatia. Muda mfupi mkawa mnagombania kisu. Yungi anataka kukunyang'anya hicho kisu na wewe unakishikilia. Na hatimaye nyote mkamwangukia pamoja Jitu aliyekuwa kamlalia Kilua. Dakika nyingine kisu kikawa kimemzama Jitu chembe cha moyo. Yeye anapapatika, na Kilua aliyekuwa kakabwa roho asitoe sauti, alikuwa amepetuka. Amerembuka. Jicho pima. Pumzi zimemwisha. Roho inammalizika kutoka. Kilua yu katika hali ya fedheha na maumivu! Na wekundu umemtapakaa nguoni mwake. (uk.202).*

Ndi- alipofungua kompyuta yake, alipata mawasiliano na bintiye Mtima aliyekuwa Uingereza. Mtima alimweleza kuwa kafungwa jela kwa kumbigija bibi mmoja wa Kizungu aliyembughudhi kila siku kwa kuwepo kwake London. (uk. 204). Hasira zilimponza na kweli hasira hasara, huenda asipate nafasi ya kuwasiliana na baba tena.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, Ridhaa anatueleza jinsi ufisadi ulivyokolea hata katika chakula cha misaada. Mwandishi akitueleza kwa kutumia methali, tabia ni ngozi ya mwili. Bwana Kute aliendeleza ufisadi hata katika chakula cha msaada. Ridhaa anasema:

*Kuna familia, kama vile ya aliyekuwa diwani wetu hapo awali, Bwana Kute, zilizofanya ujanja ili kupata mafungu zaidi. Familia moja ilijigawa, ikazaa familia nyingine mbili, zikawa familia tatu tofauti! Hatimaye Kute na aila yake waliishia kupata mara tatu ya posho ambayo wengine tulipata! Nani alikwambia kwamba hata chakula cha msaada, hata kilichotolewa kwenye madhabahu ya kidini, hakiwezi kufisidiwa! (uk. 33).*

Mwandishi anatusimulia mkondo aliouchukua Mwangeka baada ya kurejea kutoka kudumisha amani. Aliamua kununua shamba na kabla hajainunua, alifuata ushauri wa baba yake, kisa na maana alikuwa akehadaiwa mapema na kupoteza mijengo yake kutoka masoroveya walaghai na wauzaji ardhi waongo au hata kuuziwa ardhi kama mnunuzi wa pili. Hili ni dhihirisho wazi jinsi maadili ya jamii yalivyokuwa yameporomoka. Badala ya kuuzia mtu ardhi halali, anauziwa ardhi ya serikali au haramu. Mwandishi anatusimulia:

> *Visa vya watu kuuziwa hata sehemu zilizokuwa maziara vilikuwa vimeongezeka. Walioangukia mtego huu, baada ya kuchora ramani zao, walipigwa na butwaa walipowapeleka wahandisi na mafundi na kupata kuwa makaburi yamejikita kwenye viwanja vyao! Haikuwa hata ibra kuuziwa kipande cha ardhi ambacho kilikuwa tayari kimeuzwa, mtu ukapewa hatimiliki bandia, huku ile halali imetwaliwa na mnunuzi wa kwanza. Wakati unapotaka kujenga unaambiwa, "Ndugu, ardhi hii si yako. Wengine ambao hawakubahatika kugundua njama za kifisidi walidiriki kujenga majumba ya kifahari ambayo baadaye yalikuja kugeuzwa vifusi, kisa na maana, yamejengwa kwenye uwanja wa ndege au maeneo yaliyotengewa barabara. (uk. 57-58).*

Mwandishi anatueleza jinsi Lunga alivyokosa ule uadilifu wake wa uhifadhi wa misitu baada ya kufutwa kazi na badala yake akaendeleza ukataji miti na kuwa mkulima shupavu. Mwandishi anatusimulia:

> *Aliyoazimia Lunga siyo aliyoyatenda. Mara tu macho yake yalipokumbana ana kwa ana na zao la mahindi lililotamalaki kwa heba katika ekari thelathini na tano ambazo zilikuwa milki ya baba yake, moyo wa Lunga ulitwaa uchu ambao uliulemaza uadilifu wake. Tamaa ya kulima maekari zaidi ilimkumbatia, akatwaa mundu, akakata miti zaidi. Hakukumbuka kupanda mingine. Alipanda mimea mingine zaidi ya kuuza; si pareto, si mboga, vote vilinawiri katika mashamba yake. Ule wito wakuhifadhi misitu kwa manufaa ya vizazi vijavyo ulifia kwenye vilindi vya tamaa yake. (uk. 73).*

Mwandishi anatusimulia jinsi kijakazi alivyowauza watoto aliokuwa akiwahudumia. Baada ya kifo cha Lunga, Sauna aliyekuwa kijakazi aliwauza wanuna wa Umu Dick na Mwaliko kwa bibi mmoja ambaye aliwatumia katika biashara ya nipe nikupe na katika ulanguzi wa dawa za kulevya. (uk. 84)

Mwandishi anatuelezea kupitia mhusika Zohali yaliyompata akiwa kidato cha pili. Aliambulia ujauzito, akafukuzwa shuleni na kutoroka nyumbani kwa wazazi wake walionavyo kwa kuwa walimsimanga na kumdhalilisha. Zohali anatusimulia:

> *"... Nimelala kwenye barabara za jiji, pamoja na watoto wengine wa mitaani, nimetumia gundi ili kujipurukusha na hali ya ukiwa na kuumbuliwa, nimepigana na majitu yaliyotaka kuuhujumu utu wangu kwa kuninyanyasa kimapenzi. Hata wenzangu walipoona siku yangu ya kujifungua imekaribia na kunipeleka kwenye kituo cha wakfu wa Mama Paulina, siwezi kukwambia ni mangapi niliyokuwa nimeyapitia." (uk. 99).*

Zohali anaambulia mimba angali mdogo na bado uovu upo mitaani alipopakimbilia. Ubakaji na kuhujumu utu wa watu ni mazoea kule. Hata hivyo alifaulu kuokolewa na kurudi shuleni kusoma kwa kuwa alidanganya kuwa yeye ni yatima na kafiwa na wazazi miaka minane iliyopita. Hatimaye anajuta kuwa papara za ujana zilimwadhibu na kumwacha na funzo kali kwake na vijana wenzake.

Mwandishi anatuelezea kisa cha mhusika Chandachema. Chandachema alilelewa na bibi yake baada ya mama kumtelekeza na baba mzazi kuhamia ng'ambo. Bibi yake alipoaga dunia alitanga na maisha na kuamua kuchuna majani chai kujikimu. Makazi ya muda aliyopewa na Bwana Tenge na Bi. Kimai aliyashuhudia mengi yaliyodhihirisha mmomonyoko wa maadili. Anatusimulia:

> *"Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka danguro wakati Bi. Kimai alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo mbele ya macho ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kimai. Mara mojamoja Bi. Kimai angerudi bila kutarajiwa na kumshika ugoni mke mwenzake! Mwaka mmoja, miwili, mitatu..." (uk. 106).*

Mwandishi kupitia Shamsi anatueleza jinsi baba yake alipokosa lishe na kula mzizi mwitu. Madhara ya mizizi hiyo yakawa kuwa mgonjwa na alipopelekwa hospitalini hakupata dawa, ati dawa zilikosekana hospitali ya walalahoi jijini? (uk. 135) na akaishia kujifia. Naye mhusika Selume anaelezea hali ilivyokuwa mbaya alipokuwa akifanya kazi katika hospitali ya umma. Wasimamizi waliwaibia maskini dawa na kujinufaisha. Mwishowe Selume aliamua akaacha kazi na sasa ameajiriwa katika hospitali ya kibinafsi ya Mwanzo Mpya iliyojengwa na Ridhaa, ili kuwakumbuka jamaa yake waliojifia kwa cheche za moto. Hata hivyo Selume anatuonyesha jinsi serikali imekosa maadili na kushughulikia waja wagonjwa. Selume alisema:

*"Nimechoka," alijisemea siku moja, "nimechoka kuwatazama wagonjwa wakifa kwa kukosa huduma za kimsingi huku shehena za dawa zilizotengewa hospitali hii zikiishia kwenye maduka ya wasimamizi wa hospitali. Nimechoka kuongolewa kwa wimbo wa performance contract ...La kushangaza ni kwamba hata chanjo ya polio yenyewe inauziwa maskini ambao hata hawamudu kujilisha! Kufikia lengo la kuangamiza polio kunabakia kwenye ndoto za wanaozindua kampeni zenyewe. Tazama pia dawa za kukabiliana na makali ya UKIMWI na saratani. Wanaoweza kuimudu gharama yazo ndio hao hao wanaozinyakua dawa zilizotengewa raia wasiojiweza."(uk. 140-141).*

Mwandishi anatuelezea kisa kilichompata mhusika Sauna akaja kuwa mkatili na hata kulangua watoto. Sauna aliringwa mimba na baba mlezi na mama yake mzazi katika harakati ya kificha aibu anaavya hiyo mimba. Kitendo hicho cha kuavya na ukatili wa baba mlezi wa kumbaka hadi kupata mimba vinazalisha Sauna mjalaana aliyefinyangwa upya na kujipa moyo wa ujabari. Sauna alisimulia:

*"...Fikiria wewe, u kigoli, kifua ndio kinaanza kuvuvumka, kisha unaamka usiku kumpata baba yako, ba-ba-ya-ko, kwenye chumba chako cha malazi. Anakutenda ya kutendwa. Asubuhi huna uso wa kumtazamia yeyote, wala kinywa cha kumwambia mama yako kuhusu feli uliyotendewa. ...baada ya mwezi mmoja unaanza kushikwa na kisulisuli, kichefuchefu cha asubuhi nacho kinakuandama. ...(uk. 154-155).*

Sauna na Bi. Kangara wakawa mawakala wa kuwauza vijana na hasa watoto wasichana kwa madanguro, na wavulana kwa kuwapelekea matajiri ambao walishiriki katika ulanguzi wa dawa za kulevya, na wafanyakazi wa makasri ya matajiri, na katika mashamba ya mikahawa na michai.

### 4.1.6 Hali ya Kukata Tamaa na Kukosa Tumaini

Wahusika wametamauka katika harakati za kukabiliana na maisha yenye ukandamizaji na mateso. Tumaini linaweza kuwa dogo sana na mara nyingi mwisho huwa na hali ya kutoaminika na kuonyesha kuwa mabadiliko ni magumu sana kufanikisha. Wahusika hukata tamaa juu ya mustakabali wa maisha yao. Hali kama kifo cha mzazi, umaskini,

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* Akida alifiwa na mama yake aliyeangamia katika ajali ya barabarani. Kifo cha mamake Akida kilikuwa pigo kubwa kwake kwa sababu aliishi kwa huzuni na mlezi kwa miaka mingi. Tunaelezwa kuwa:

*Zaidi ya miaka kumi tangu mama kufa, bado nahisi uchungu moyoni kila nikimkumbuka. Laiti mama angalikuwapo leo, ashiriki furaha na fahari yangu. Nakwenda Tandika kwa mara ya Kwanza maishani mwangu. Hilo si dogo. Mama asingaliliona dogo la mwanawe kwenda kuzuru jiji kuu la nchi yetu Kiwachema...Nakwenda jijini kuzawadiwa na waziri... Mama! Mama! Laiti ungalikuwa hapa utabaruku katika furaha na fahari yangu. Mama! Ni hapa Tungule ndipo ulipofia (uk. 1).*

Ukosefu wa mama mzazi katika hafla yake ya kuzawadiwa jijini Kiwachema, kunamkumbusha Akida kifo cha mwalimu wake Alex aliyerukwa na akili na siku moja akapatikana amekufa. Kabla kifo chake, mwalimu Alex angesema wazi kwa umma na siku zake za mwisho angehutubia vichaka na kusalimu hata ng'ombe. Mwisho wake duniani uliwahuzunisha wengi kwa kuwa hawakuweza kumwokoa wala kumtibu mwalimu Alex. Akida anaeleza:

*Hapo ndipo nilipoiona maiti ya mwalimu wangu mpendwa Alex. Ilikuwa imekatwakatwa vibaya. Umati wa wanakijiji waliokusanyika kwenye kingo za mto uliachama. Nilihisi huzuni. (uk. 4-5).*

Akida anakumbwa na huzuni kila mara anapomkumbuka mama yake. Mbali na kuhuzunika, kijana huyu ameachiwa jukuma la kumtunza baba yake ambaye alikuwa anaugua. Ugonjwa na na kumhudumia mzazi ni mzigo mzito sana kwa mtoto huyu. Tunaambiwa:

*Mama katuacha mikono miaka kadha iliyopita, baada ya basi alimokuwa akisafiria kugongana na lori. Baba alikuwa naye kavimba miguu, sijui kwa matende au maradhi gani. Dhima ya kumtunza iliniangukia. Haikuhalisi kumwacha baba peke yake na kwenda kujifurahisha nafsi yangu jijini (uk. 10).*

Mwandishi anatueleza jinsi Akida anavyokata tamaa ya maisha na hata kama mambo mazuri yametendeka kwake na baba yake rohoni anakosa matumaini. Akida anasema:

*Nimetingwa na mawazo tele. Jana tu nimemwona waziri, nikamsalimia mkononi, akanipa zawadi. Sasa simfikirii. Jana tu zawadi yangu, nisiyopata kuijua ilikuwa nini, imepotelea garini. Lakini sasa siifikiri. Jana jioni nimelimbuka kujiona kwenye kioja kiitwacho runinga*

*nikipokea zawadi kutoka kwa waziri. Lakini linifikirishe nini hilo? Jana tu nimeshuhudia ufanifu wa babangu katika fani ya uandishi; sikuona tu, nilipewa nakala za kitabu chake kilichochapishwa kumpelekea. Ila sasa fahari hiyo naiona ombwe tupu. ...Sijalala usingizi, nimejilaza tu kitandani. (uk. 58).*

Tim na Akida wanaposikiza Idhaa ya Kiswahili ya BBC inawapasha habari ambazo walikuwa wamehofu, zinakatisha tamaa ya maisha:

*"...Habari zinazotufikia hivi punde, "alisema mwanamke mtangazaji, "zasema, mamia ya watu wameonekana wakikimbilia usalama –wengine wao kwa miguu kwenye miji mbalimbali nchini Kiwachema, baada ya kufumuka vita vya kikabila katika Wilaya ya Korosho nchini humo. Mwandishi wa BBC aliyeko Tandika, Jiji kuu la Kiwachema, amearifu kuwa watu takribani thamanini wameuwawa na mia tatu wakajeruhiwa, wengine vibaya sana, katika vita baina ya makabila ya Wakorosho na Wakanju vilivyoanza siku chache zilizopita. (uk. 60-61).*

Katika gazeti alilokuwa amelinunua Tim, mle ndani kulikuwa na habari ya mzee mmoja ambaye walikuwa wamekutana na Akida pale jijini Tandika katika Kampuni ya Mawakili Gembo na wengine. Habari ya mzee huyo ni dhahiri kuwa alikuwa amekosa matumaini ya kuishi baada ya kukosa fidia ya ajali. Mzee alikata tamaa ya kuishi na kujitoa uhai. Habari yenyewe ilisoma ifuatavyo:

*"Wananchi wanautazama mwili wa Yusuf Matuko (60), aliyejitupa kutoka ghorofa ya 22 ya Tembo House baada ya wakili wake Bwana Tony Gembo kukataa kuonana naye juu ya malipo ya bima ya ajali iliyotokea miaka 10 iliyopita. Hayati Matuko, aliyehasiriwa katika ajali hiyo, yasemekana alitorokwa na mkewe baada ya ajali hiyo. Jitihada zake za kudai malipo ya bima hiyo zimekuwa zikigonga mwamba na wakili wake kumvinjari..."(uk. 62)*

Ujio wa Tamari, Tamari kumfokea Akida kuwa yeye ni Mkanju na kufutwa kwa kazi kwa Tim maana alienda sherehe ya Akida ni mambo yaliyomsonga Akida asubuhi moja. Akida akatoka na kuzurura Jijini Tandika. Mawazoni mambo mengi yalimpitikia. Hana wa kuelezea ila kujiamulia lililo bora:

*Nitawahi kwenda Shule ya Kitaifa ya Upili ya Kiwachema nilikopewa nafasi? Nitasoma niwe msanifu ujenzi maarufu nchini? Au matamanio yangu yameyeyushwa na kutokomezwa na vita vilivyozuka kwetu kijijini. Nipande ghorofa nijitupe kama Mzee Yusuf Matuko? Au nijitupe mbele ya gari liendalo kasi? Nilale reli nisagwesagwe na treni? (uk. 65)*

Tim na Akida wanakosa wazee wao hospitalini lakini kisadfa wanamkuta Mzee Uledi. Mzee Uledi anawaeleza alivyotoroka. Anawasimulia jinsi alivyokuwa amemtembelea Mzee Sululu ampigie gitaa. Ghafla bin vuu walijuzwa kuwa jeshi la Wakorosho linatoka ng'ambo ya Mto Kibisi kuja kuwavamia. Wanasimulia:

*Mzee Sululu alibakia kwake na makisio ya Mzee Uledi ni kuwa huenda aliuwawa. Tim na Akida walimwacha Mzee Uledi na wakapiga sachi wodi nyingine. Sachi yao iligonga ukuta tu. Wakakata tamaa ya kuwapata wazee wao na kutoka na kwenda zao (uk. 79).*

Akida na Tim wanapoondoka hospitalini, wanampata mwanamke mmoja akilia kwa kuwa mumewe aljifia juu ya machela kwa kukosa huduma za daktari.

*"Sasa n'tafanya nini jamani kaniacha mume wangu?" (uk. 79).*

Yule mwanamke alishtakia hali yake umma usio na uwezo wowote – alikata tamaa na kukosa matumaini kwa sababu juu ya machela mgonjwa mwenyewe kanyooka, kalala usingizi, usingizi usiojua wakati wa kuamka. Akida anavalia kaptura badala ya suruali ndefu kuashiria nchi yao ina msiba wa kuongozwa vibaya. Jerumani anasema:

*Utakuwa mtu mzima lini Herr Madodo? Alijibu. 'Unapaswa kujiuliza Kiwachema twendapi? Kiwachema ni nchi yetu ati. Tuwapeje nyadhifa wafisadi, wabaguzi na wapenda ukabila? .... bendera hupeperushwa nusu mlingoti wakati gani?...sio wakati wa msiba? Suruali kipande hii naivaa kama kwamba bendera nusu mlingoti, ishara ya msiba. (uk. 163)*

Katika *Chozi La Heri,* Dickson alitii hali yake kwa kukosa mlezi na shuruti zake kijakazi Sauni na kulangua dawa za kulevya zake Buda. Msimulizi anasema, kisha Dick anajisemea:

*... na asiwe vipi mwanagenzi, kinda wa miaka kumi kuingizwa katika biashara ya aina hii? Zipo siku alipotetemeka nusura ajisaliti. Lakini alizoea kujipa moyo. Kila mara alipopatwa na kiwewe alijiambia, "Dickson, wewe jikaze,. Mzee wako hayupo hapa, amejipumzikia ahera. Na mama yako hakuwapo tangu hapo. Angekuwapo asingekuacha kutimbwa na ulitima." (uk. 119)*

Barua ya Nana, bintiye Mzee Muyaka ni ya kukata tamaa na kukosa tumaini kwake na kwa mama yake Bi. Tina kumwona mchumba wa mwanawe. Barua ilitufahamisha hayo:

> *...Tangu kufanya uchumba na mchumba wangu, sikuwahi kufikiria kuwa mtengo ungeweza kujiri. ...Ila sasa mbele hakwendeki. Pamepita hitilafu kubwa kati yangu na mchumba wangu. ...hatutakuja nyumbani kwa shughuli ya posa kama tulivyokuwa tumepanga. Niombee Mungu anipe subira wakati huu wenye utata. (uk. 179-180).*

Vijana kama Dick, baada ya mama yao kuwaacha na baba kujifia kwa msongo wa mawazo hawana budi kuuza dawa kwa kujisajiisha na maovu ya dunia. Licha ya umri mdogo aliamua na liwe na liwalo atasafirisha dawa za kulevya.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Ndi- anatusimulia jinsi wananchi waliosalia ni kama magonjwa tu. Dhihirisho la kukosa matumaini.

> *Lakini wote ni wawele, ingawa si wagonjwa wa dhahiri. Ndiyo wanakusikia ukisema, lakini hawasikilizi wala hawasikii. Hawakuduhushi. Wanatazama lakini hawaoni. Wanaonekana watu wenye nadhari lakini hawapimi. Hii ndiyo hatima ya uhuru wetu wa miaka arubaini na mbili. Sote tumekumbwa na ugonjwa wa ajabu unaotuangusha kwenye maweko ya chini kabisa ya mwanadamu awezako kuangukia. Ajabu! Sisi ni wau tuliokuwa zamani imara, watundu, watetezi wa nafsi zetu, wapigania heshima ya nchi yetu, watu tuliosimama kidete kwa miguu yetu isiyochoka – kwa fahari na kujisifu! U wapi wakati ule katika dunia yao! (uk. 2)*

Shogake Mtima T'uu aliposhindwa na maisha Uingereza alirejea na pamoja naye alikuwa na zawadi ya Ndi-ambayo ni kompyuta. Punde tu T'uu aliporudi kwao, alifariki. Kwao pia kulimshinda na kumkatisha tamaa (uk. 6).

Ndi- anatueleza kuwa kuna aina mbalimbali ya kazi. Unayoifanya ifanye kwa ari na ukakamavu hata hivyo enzi zile sio za sasa. Anatuelezea kuwa huenda labda aliathirika na mawazo ya vitabu na alichokidhania wakati ule sasa amekosa matumaini:

> *Nilimhusudu Robinson Crusoe aliyetaka kuketi na kukita katikatiya ngazi ya maisha. Siku hizi ndiyo kwanza nitambue kumbe ile ilikuwa ndoto. Wakati wa Crusoe ulikuwa mbichi. Wakati wa kila kitu cha sasa kilipokuwa majimaji bado, kikioteshwa na kutoa mizizi. Wakati wangu ni wakati wa kila kitu kinapoanza kuoza. (uk. 18)*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatueleza jinsi Ridhaa alivyojipata Msitu wa Heri, amesoma, amehitimu na kuwa daktari aliyewaponya wengi. Amewasaidia watu kule ilhali wamemfanyia madhila ya kuichomea familia yake ndani ya nyumba. Ridhaa anajisaili kwa maswali mengi tu kuonyesha ametamauka na watu pale Msitu wa Heri:

> *Lakini ni kipi kilichosababisha hali hii? ...Je, huu si mchango tosha wa mtu kuitwa ndugu hata ingawa mgeni? Kweli jaza ya hisani ni madhila? Vipi watu wawa hawa walioniita 'Ndugu' na 'Mzee', tukala na kunywa pamoja, tukazungumza ya kupwa na kujaa wananilipulia aila na kuyasambaratisha maisha yangu?" (uk. 12)*

Mzee Kedi alimsaidia kupata shamba pale, Mwanawe Mhandisi Kombo ndiye aliyesimamia ujenzi wa nyumba yake. Wake wao wamekuwa marafiki na kadhalika. Lakini moto ulipokuwa ukichoma aila yake alisikia Terry akipiga usiyahi, Uuui ...Mzee Kedi, usituue, sisi tu majirani! Maskini wanangu! Maskini mume wangu! (uk. 3). Anaamini sasa kuwa Kedi alichangia katika ule moto wa mauti. Kinyogo cha ulowezi kilimletea balaa Ridhaa hata kama alikuwa anaishi nao kwa amani. Sasa amekosa tumaini maishani.

Ridhaa anatueleza waliosababisha fujo katika vita kati ya wafuasi wa Mwekevu na mpinzani wake. Ni vijana wa vyuo waliomaliza masomo na kukosa kuajiriwa. Waliongozwa na 'Hitman'. Vijana wanasimulia yaliyowasibu yanayoonyesha ukosefu wa matumaini ya kazi na tija ya kila siku. Wanasema:

> *" Mnatuhadaa na vishahada mnavyotupa vyuoni, vishahada ambavyo ni laana kwetu, tanuri hasa linalouchoma uwepo wetu. ...Mtu anahitimu hata digrii tatu, kisha anapiga lami miaka kumi bila kuwaza kuwa anaweza hata kujiajiri. ...Hapa ndipo unashangaa utarudi kwenye shamba lipi na tangu hapo familia yako uliiacha ikiishi kwa msaada wa wale wale waliotoka mbali kule walikotoka, wakapewa maelfu na maelfu ya ekari, wakajenga viwanda na maduka ya biashara, wengine wakalima mashamba makubwamakubwa huku wakidai ni njia ya kuwahakikishia wenyeji hali ya kujitosheleza kwa chakula. Kumbe wanakuja kutufukarisha zaidi! Tunapolalamikia kashfa za unyakuzi wa hata vikata vidogo tulivyo navyo tunapozwa roho kwa, 'Tumeunda tume ya kuchunguza kashfa hii. Waliogawiwa au kununua mali ya umma kwa njia ya udanganyifu watakabiliana na mkono thabiti wa serikali.' Ni wazi kwamba mwananchi wa kawaida hadiriki kuziona ripoti za tume hizi au tuseme ripoti hizi huwa wageni wa rafu za Makavazi ya Kitaifa!" (uk. 21-22).*

Mwandishi, kupitia Selume na Meko walio wauguzi hospitali ya Mwanzo Mpya wanatuelezea kisa cha mgonjwa mmoja aliyekufa kwa kujihusisha na pombe haramu baada ya kuhitimu chuoni. Mwanafunzi huyo alikuwa wa shahada ya uzamili lakini kutokana na hali duni ya maisha vyuoni na gharama ya masomo kuwa ghali, nayo halmashauri ya elimu inayotoa mikopo ya masomo haimudu kutosheleza mahitaji ya wanafunzi wanaohitaji mikopo na ruzuku wanaishia kunywa pombe haramu kwa kukosa matumaini. Matokeo ni vifo visivyotarajiwa wala kupangiwa. Selume anaelezea zaidi kuwa wengine hunywa pombe hiyo kwa sababu familia zao huwa tayari zimesambaratika (uk. 142).

### 4.1.7 Uasi na Mapambano Dhidi ya Mfumo

Wahusika wakuu wanajaribu kupinga na kubadilisha hali iliyopo, ingawa mara nyingi wanakutana na vizuizi vikubwa na hatari kubwa. Juhudi za wahusika na harakati za kubadili maisha yao unawatuma kufanya bidii na kujiopoa kutoka umaskini na kupinga mifumo ya kitamaduni na kijamii kwa gharama kubwa.

Katika *Kufa Kuzikana,* Akida na Tim ni marafiki wa kufa kuzikana ilhali wanatoka katika makabila tofauti. Akida ni mkanju naye Tim ni Mkorosho. Makabila haya mawili yana uadui mkubwa lakini vijana hawa wawili wameamua kuwa ukabila hautakuwa kikwazo kwao na watashirikiana kuukomesha. Akida anapofaulu katika mtihani wake na kutakikana kwenda jijini kuzawadiwa, Tim aliyeishi jijini Tandika alikubali kukaa naye mpaka amalize shughuli zake za kuzawadiwa jijini. Tamari, dadake Tim alikuwa akimchukia Akida kwa sababu si wa kabila lao tangu utotoni. Akida anasema:

> *"Tamari aliniona kama mkia wa mbuzi, kuzaliwa kwangu hasara kwa dunia" (uk. 8)*

Akida anaeleza kuwa hawana uhuru ingawa inasemekana wazalendo walimwaga damu yao ili aondoke mkoloni. Haki za kusema na kuamua zimedhibitiwa lakini wamo mbioni kuasi mfumo huo dhalimu. Tunaelezwa:

> *Na u wapi uhuru usemwao ulipatikana kwa wazalendo kumwaga damu yao ili mkoloni aondoke? Au tuseme jana ilijipatia uhuru wa kumhini mtu binafsi uhuru wake? 'Hii ni dhuluma, 'alitamka Pam. (uk. 56).*

Mwandishi anatueleza kuwa Tom, mtoto wa pekee wa Mzee Mangala alioa mzungu baada ya kutoka Marekani. Tim anaelezea Akida kuwa wawili hao walifanikiwa kuishi Mtaa wa Milimani jijini. La kushangaza ni kuwa hawana watoto. Tim anamwambia Akida kuwa Tom hamfuchi chochote na ndiye aliyempa habari hiyo. Huyu mwanamke mzungu aliitwa Jenelle na katu hawataki wazae. (uk. 59). Huu ni uasi na kupinga mifumo asili ya ndoa. Tom aliyekuwa mkurugenzi wa Anken, shirika moja lisilo la serikali na kutononokewa na hela hana mtoto.
Wahusika Tim, Akida na Tamari walifanya kazi ya kila aina aghalabu wapate kitu cha kutia tumboni. Tim aliwapiku kiumri aliwaongoza ili wasije wakazembea. Chakula kilikuwa haba, cha mshindio na wakati mwingine walilala bila kula chochote. Akida anatueleza:

> *Hapakuwa na nafasi ya kuzembea, kila mtu alpaswa kuzumbua riziki. Tim na mimi tulirauka alifajiri kwenda kukoroga zege, kuchimba mitaro, kubeba magunia ya mazao sokoni, kusukuma rukwama, kufanya utopasi na kadhalika, muradi turejee nyumbani na chochote. Tamari ambaye alikuwa akipata nafuu alikwenda kuwafulia matajiri nguo majumbani mwao na kuwapigia deki maadamu tu aje nyumbani na chochote. (uk.119).*

Akida alisingiziwa na Tamari kuwa alikuwa karibu kumbaka. Badala ya kujitetea mbele ya Tim, aliondoka na kutanga ma Mtaa wa Falkland. Alifika katika kikao kimoja ambapo vijana walikuwa wakibugia *busaa.* Akida aliketi kujituliza mawazo baada ya uongo wa Tamari. Hapo ndipo aliposikia mlevi mmoja akiridhia na kujisifu jinsi alikuwa amewauwa Wakanju. Alijasiria na kumsubiri huyo muuaji wa Wakanju alipoenda maliwatoni ndipo alimgonga na kipande cha mti akamuua. Sadfa ikawa ni Mzee Zablon aliyekuwa amemwona awali pale Baraki akiwaongoza wahuni kuwaua Wakanju nusura Tom ajifie walipomvamia. Akida anatusimulia:

> *Moyo wangu ulitweta, ukatuta na kurindima kuliko wakati wowote mwingine katika maisha yangu yote. Nimemwua mtu. Sikuwa na shaka kwa kuwa nimemfisha Mzee Zablon, babake rafiki yangu Tim. (uk. 133)*

Kisa cha Jerumani ni dhihirisho wazi wa mapambano dhidi ya mifumo. Jerumani anamwelezea Madodo Kipande – Akida, sababu ambayo aliwekwa gerezani ilikuwa kumtetea mwafrika mwenzake na baada ya kula kalenda akafurushwa kuja kwao Kiwachema na kunyang'anywa ufadhili. Jerumani alisimulia:

> *"...Wajerumani wameendelea lakini wanamchukia mtu mweusi. Mtu unaonewa tu kwa sababu ya rangi ya ngozi yako, ushafahamu? Nilikuwa nasomea uhandisi katika Chuo Kikuu cha Koln, nimo mwaka wa pili. Nikawaona skin heads wanne wanamshambulia mwanamke mweusi burebure akiwa na kitoto chake kidogo nje ya Cafe Charmante. Sioni dhulma nikatulia. Nikawarushia ngumi nzito kama mwendawazimu. ...Nikapandwa na madadi. Nikaukamata mtaimbo niliouokota pale chini nikamzaba skin head mmoja kichwani. Akadondoka kama dumu la maji...Nilikamatwa. Katika kufuatia haki sichelei hata*

*kuua mie." (uk. 155).*

Mhusika Jerumani aliyekatiza masomo yake huko Ujerumani, alivuta bangi, sigara na kulewa pombe ili kujipoza. Akida anaeleza aliyoyaona alipomtembelea:

> *Alinitungia macho na kutikisa kichwa. Waniona hambe sio? Au unafikiri bangi imenizidi? Njoo kwangu leo jioni nikuonyeshe... Ukutani kulikuwa na picha kuukuu ya mbunge wetu Johnstone Mabende, macho yametobolewa mashimo. Aidha harufu ya sigara ilichanganyika na ile ya pombe aina ya gongo tokeo likawa mseto wa kukirihisha (uk. 157)*

Matatizo ya dawa za kulevya na unywaji wa pombe yamekuwa majanga makubwa duniani kote. Wanajamii hasa vijana wameathirika pakubwa. Vijana wamekuwa ndio mkondo wa kutumia, kuuza na hata kusafirishia dawa za kulevya. Dawa hizi zina athari ya kuvuruga akili na kuleata msongo wa mawazo. Hata huishia kwa vijana kuwa wabakaji, majambazi na hata wauaji. Jerumani anamweleza Akida haya:

> *Hii nchi yetu inahitaji mapinduzi. Sio mapinduzi ya Serikali, mapinduzi ya mitazamo, misimamo na mikabala. Sisi Wanakiwachema tumelemaa vibayavibaya. Subiri msimu wa tohara ufike uone maajabu. Utawaona wasichana maskini wanalazimishwa kutahiriwa burebure. Wengine watapatwa na blutung wafe. Mwaka jana wamekufa wawili. Lo! Mila gani hizo za upuuzi? Ndio maana tunabaki nyuma. (uk. 154-155)*

Jerumani anamhamasisha Akida kuhusu mapinduzi dhidi ya mfumo mbaya. Anamzindua na kumuasa wapigane na mila potovu kama kupashwa tohara kwa wasichana. Ilibidi wasichana wengine watoroke usiku wa manane iliyo na hatari zake. Akida anaeleza alivyojaribu kumwokoa Cynthia:

> *Dada zangu wote wakubwa wametahiriwa. ..Zamani nilifikiria ni sawa lakini sasa sitaki. Nasikia kuna madhara. Wasichana wengine wawili walifariki mwaka jana pale ng'ambo. ...Sikuwa mweledi wa kuendesha baiskeli wala baiskeli yenyewe haikuwa na kurunzi. Nilimwangusha Cynthia mara tatu hivi. Ulikuwa mwendo wa kilomita arubaini hivi (uk.170).*

Polisi na wanafunzi wanakabiliana kwa sababu ya maovu vyuoni. Wanafunzi wanajitetea kuukomesha unyama na kuleta mabadiliko katika idara ya polisi. Redio ya idhaa ya Kiswahili ya BBC ndani ya basi inatangaza:

> *BBC walisema katika taarifa yao kuwa chuo Kikuu cha Tandika kilifungwa baada ya polisi kutiba maandamano ya kupinga kitendo cha polisi cha kumwua mwanafunzi mwenzao katika hali isiyoeleweka. ...na ukiwa mwanamke wakati wa rabsha ndipo unapotamani ungalizaliwa mwanamume, alisema yule mwenzake msichana. 'Kwa sababu ya mwanafunzi wa kike ndiye shabaha ya askari polisi mwenye uchu. Sio?' Alisaili mvulana. 'Bila shaka leo mimi mwenyewe nimeponea tundu la sindano tu,' msichana alisema. (uk. 138).*

Wanafunzi wanapinga uovu wa polisi kwa kushiriki maandamano.
Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Mtima, bintiye Ndi- anamweleza baba kupitia barua jinsi ya kuishi ughaibuni hata kama mwenyeji wako amechoka nawe. Amejasiria kuishi na kupambana na hali yake hata kama nafuu aliyoifuata imezongwa na wingu kubwa la wasiwasi. Mtima aliandika:

> *Lakini utafanyaje unapokuwa huna pahala pengine pa kwenda? Unachuna uso. Unalazimisha mambo. Unajitia ukavu. Ndiyo maisha ya huku; kama unaweza kuyaita maisha. Nyumba nasikia nitapewa na 'mama' – yaani 'Malkia Elizabeth'....Maana mwanzo wowote ni mgumu (uk. 7)*

Ndi- alikuwa na mazungumzo na bintiye, Kilua. Kilua anamuuliza swali. "Kwa nini mtu huingiwa na wazimu?" (uk. 91). Ndi- hakuweza kumjibu kilua na badala yake alikuwa na monolojia kuelezea sababu za kuingiwa na wazimu. Maelezo yake yanaafiki uasi wa mifumo. Ilhali kilicho wazi ni kuwa Ndi- si wazimu bali hana mshahara wala nguvu tena ya kuikimu familia yake Uzungumzi nafsia wa Ndi-:

> *Kumwambia kwamba wazimu maana yake kwenda kinyume na watu wanavyoona – wengi au kiganjatele. Kuishi ukisononeka kwa dharau yao. Kwa sababu umeamua wewe kuwa wewe si wewe wao. Kwamba umeweka mpaka wasioutaka baina ya wewe na wao. Inavyotakikana ni kwamba ufuate njia wanayokanyaga wao. Lazima uelekee wanakokupeleka wao. Ingawa unajua njia yao ni ya maangamizi. Sababu ya wazimu ni kukataa. Kususia. Kupinga! Kukataa kukubali kila kitu. Kukataa kuridhia na kuitikia "ndiyo" kwa kila jambo. Nilitaka kumwambia kuvua nguo maana yake ni tambiko la kurejea katika asili ya ubinadamu. Kujikashifu wewe mwenyewe na kuukashifu utu wetu kama unavyokashifiwa katika maisha yetu ya kila siku. Kama jamii ilivyokwisha kashifika kwa uzito wa kasheshe! Kuvua nguo ni kuhakikisha usafi wa kweli si ubandia na unafiki. Kukung'uta magwanda yote ya taka unayovishwa na jamii tokea unapozaliwa. (uk. 91)*

Ndi- aliyavua magwanda kuukashifu utu na watu warudie nyenzo za kale zilizokuwa bora na sio kupotoka na kuporomoka kwa njia geni hasi.

Baada ya mafuriko yaliyojenga bahari ya ghafla, Ndi- anaogelea na anapofika kina cha mabli anamkuta Uledi. Uledi anamwongoza hadi chumba kimoja ambapo mna wanawake wanne. Bi. M, Bi. Mize, Biti Jabu na bintiye Yungi. Wanamkosha kwa maji na kumweleza kuwa alikuwa ameumia kwa kuogelea nchi kavu. Lakini ombi lao ni moja kuwa awe mtetezi wao kwa sababu yeye ni mwandishi maalum. Ndi- anasimmulia aliyoambiwa:

> *Nilimsikia tena Bi M akisema, "Wewe ni mwanamme wa mwanzo kuoshwa na wanawake. Tena wanawake watatu. Mmoja mkeo, mwingine rafikiyo wa kisanaa na mwingine rafiki wa uwananchi. Nadhani hutalisahau jambo hili maisha. Huu ni usuhuba maalum na wanawake. Kwa lolote unalotaka kufanya kumbuka nguvu maalum za wanawake kwa faida ya watu wa nchi hii, wake kwa waume!" ...sheria zinazohusu haki za watu wote, kanuni zisizofaa kuhusu watu wote. (uk. 185).*
>
> *Ndi- anakutana na watu karibia kumi na watano walioasi ubadhirifu wa serikali. Hii ndiyo sababu sasa yu taabani ya uhitaji wa hela. Bi M sasa inambidi achuuze chakula ofisini kuikidhi familia yake. (uk. 188)*

Mwandishi anatueleza kuwa Yungi anakuwa mstari wa kutetea ardhi yao wasije wakanyang'anywa. Yungi amechaguliwa kama kiongozi wa eneo lao kukutana na wakazi. Bi M anamwelezea Ndi-:

> *Serikali inaona afadhali iwafanye wananchi wao wakimbizi kumfurahisha mgeni. Yungi wanalipinga hili na dada zake Mtima na Bisudi, wanapata jina la kuwadunisha 'waletafujo. Hata hivyo harakati zimepamba moto za kujinasua na serikali dhalimu. Kesho sherehe itapangwa ya kusherehekea dunia yetu:...Si inajua kwamba wanataka kuvunja nyumba za eneo letu hili lote na kujenga hoteli ya Wataliana? (uk. 210)*

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi anatusimulia jinsi Ridhaa hakuzika majivu ya aila yake bali aliyaacha pale. Hata Mwangeka anaporejea anamuuliza babake kwa nini hata hakuzika majivu katika kaburi la jumla – *mass grave*. Ridhaa alimjibu:

> *"Kuna mambo ambayo sharti yatendeke kinyume na kaida za kimaumbile; si lazima maisha ya binadamu yafuate kanuni zilezile kila mara. Wakati mwingine nadhari ya binadamu hutulia tu pale anapodengua hali. Sijui kama kijana umesoma ile nadharia ya Deconstruction. ..." (uk. 52)*

Mwandishi anatusimulia jinsi Lunga alivyofutwa kazi akiwa mkurugenzi wa kitengo kilichoshughulikia uhifadhi wa nafaka katika Shirika la Maghala ya Nafaka. Lunga alipinga serikali kuuza mahindi aliyoyahofia kuwa yameharibika. Baada ya kufutwa kazi akawa mkulima stadi. Marafiki zake wamempa jina la msimbo *Mkulima Namba Wani.* Hata kama ni mkulima stadi, tunaona kuwa ameasi mfumo wake wa awali akiwa mwanafunzi wa kutetea mazingira. Mwandishi anatusimulia:

> *Hakuwa na chochote baada ya kupigwa kalamu na kufukuzwa nyumba ya kampuni. Sasa anamiliki, si nyumba tu, bali pia mashamba makubwa. Anafuga kuku, bata, mbuzi na ng'ombe. Anaweza kuwaajiri watu kufanya kazi katika mashamba yake. Sasa Lunga ni Lunga Kiriri. ...Ulimwengu umenifunza kutumia fursa niliyo nayo kuyaboresha maisha yangu. Mungu mwenyewe alitupa ulimwengu tuutawale, sio ututawale; rasilimali tuitumie wala si kuifumbika ardhini kama kiasi kitamu. Tusije tukawa kama yule mtumishi kwenye kitabu kitakatifu ambaye alichimbia talanta chini badala ya kuizalisha! (uk. 73-74).*

Mwandishi anatueleza kuwa baada ya kifo cha Lunga na kupotea kwa wanuna wake Umu, Dick na Mwaliko, Umu aliamua kugura kuenda jijini kuwatafuta wanuna wake. Umu aliugura Mlima wa Simba na kuelekea jijini. Kisadfa alimkuta Hazina aliyemwonyesha hisani mapema. Leo ilikuwa zamu yake kusaidiwa na ndipo mama yake Hazina, Julida alimpangia akapata makao na kisomo katika shule ya Tangamano.

Mwandishi anatuelezea athari za mapambano ya mfumo inavyomwathiri mgonjwa mmoja aliyelazwa kituo cha afya cha Mwanzo Mpya. Kipanga akawa mlevi na kunusurika kifo kwa mambo ambayo hakuwa na uwezo kuyatatua. Kupitia simulizi za Selume tunapata kisa cha ghulamu mmoja aliyeitwa Kipanga:

> *Kuna huyo ghulamu Kipanga, anayepokea huduma za ushauri nasaha hapa petu. Yeye alinusurika kifo kutokana na kangara iliyowaua watu sabini mwezi uliopita. Huyu anasema kwamba alianza kuchovya kidogokidogo akiwa kidato cha pili baada ya aliyedhania kuwa baba yake kumkana, na kulazimika kuhama alikoita kwao, yeye, mama yake na mnuna wake ambaye alisemekana ndiye mwana halisi wa baba yake. Kipanga anasema kwamba lililomuuma zaidi ni kwamba alipomtaka mama yake kumwambia ukweli, mama mtu hakumpa jawabu la kuridhisha. Alichosema ni, 'Yapo mambo ambayo mtu hawi na uso wa kumtazamia mwanawe kwayo. Anayekulea ndiye mzazi wako, mradi tu akubali kuwajibikia ulezi.' (uk. 143)*

Mwandishi kupitia Selume wanaelezea mhusika Tuama anayeasi usasa na kupashwa tohara nusura afe kwa kupoteza damu nyingi. Selume anaelezea kisa kingine cha mgonjwa aliyeitwa Pete ambaye aliposwa na wajombake kwa Bwana Fungo na kutoroka ndoa hiyo na mwana mmoja. Baadaye Pete alijiingiza kwa uhusiano mwingine na Nyangumi uliomwongezea kinywa zaidi cha kulisha. Baadaye Pete anauasi uhusiano na Nyangumi na kuwa mjamzito na mlevi mmoja alipokuwa akiuza pombe kwenye klabu. Hali ya kuwa na wana watatu na hamna mlezi mwenza inamfanya Pete kujaribu kujiangamiza kwa kunywa sumu ya kuua panya lakini bahati aliokolewa ndiposa alijikuta akihudumiwa katika kituo cha afya cha Mwanzo Mpya.

Mwandishi anatusimulia kisa cha mhusika Mwangemi na Neema ambao hawakuwa wamejaliwa kupata mtoto. Neema anakumbuka kisa cha kumwokota mtoto na kumkabidhi kituo cha *Benefactor* siku za awali. Baadaye Mwangemi, mume wake anampendekezea kupanga mtoto maana waliyejaliwa alikufa kwa ugonjwa wa *Sickle cell*. Neema anapokubali maoni ya mumewe wanafaulu kumpanga Mwaliko na kumlea kama wao kwa tunu, tamasha na nidhamu (uk. 167). Wahusika hawa wawili wameasi utamaduni na kumpanga mwana ambaye hawakumzaa.

### 4.1.8 Udhibiti wa Mawazo

Vidhibiti hutumika kufuatilia jinsi watu wanavyofikiria na kuamini. Udhibiti huu unalemaza masuala muhimu kama dini, uchumi, utamaduni, mawasiliano uhuru wa habari na elimu na hutumiwa kuhakikisha kuwa watu wanafuata fikra za kikundi chenye nguvu na kinachodhibiti mawazo ya wananchi.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* waliopasha Tom habari kuhusu kwao Baraki wanadhibiti mawazo yake kwa kumweleza jinsi kule kumeharibika hakuendeki kamwe. Mwandishi anasema:

> *"Watu waliotoroka vita Baraki wamemwarifu Tom kuwa vita vimechacha. Wakorosho na Wakanju wanauana tuputupu. Miili ya watu waliochinjwachinjwa inaonekana ikielea kwenye Mto Kibisi. Nyumba zinateketezwa kiholela, za Wakorosho na Wakanju kadhalika. Wanawake wanabakwa. Na waandshi wa habari wamezuiliwa kuingia Wilayani Korosho, ulimwengu utajuaje yanayoendelea huko?" "Habari zozote kuhusu familia zetu?" "Sijasikia lolote. Tom asema familia zimetawanyika – kila mtu akakania kuiopoa nafsi yake. Watoto wametelekezwa na wazazi wao, wake wametengwa na waume zao. Baadhi yao wamekimbia Jijini. (uk. 59).*

Haya maelezo yalituchorea taswira ya mambo mabaya yaliyokuwa yakiendelea pale Baraki. Mbali na vita vya kikabila maovu kama ubakaji, mauaji, kuvunjika kwa familia na hata ukosefu wa habari vinawapa Tim, Tom na Akida msongo wa mawazo iwapo jamaa zao waliosalia kule wako salama au tayari wameuawawa.

Katika harakati za Tim na Akida kuwatafuta wazee wao walipoelezewa kuwa baada ya vita vya kikabila, watu na familia zilitawanyika walienda Hospitali ya Rufaa Tandika. Walifika wakati wa kazi na bawabu kuwakataza kuingia. Walipofukuzwa na kuambiwa wangojee muda wa kuwaona wagonjwa, Akida alimpa hongo ili awaruhusu. Hili ni dhihirisho wazi kuwa ufisadi na hela zinadhibiti mawazo na uvunjaji wa sheria. Akida anatueleza mtagusano na kati yao na bawabu:

> *Saa za kuwaona wagonjwa zimepita. ...bawabu alifoka. Msiniharibie kazi. Nimekuambieni nendeni. Tulinywea na kuanza kupiga hatua mbili tatu hivi kwenda zetu. Radi ilipasuka huku mvua ikiongezeka. Nikamrejelea bawabu, nimefumbata noti ya shilingi ishirini mkononi. Nikamsalimia bawabu kwa mkono huo na kumwachia hela hizo alizozitumbukiza mfukoni mwake kwa kasi ya umeme. "Piteni basi," alituashiria tupite na kutufungulia kilango (uk73).*

Tom, mtoto wa pekee wa Mzee Mangala aliporejea kutoka ng'ambo, mbali na kuwa na kasri jijini alijenga kwao kijijini kulingana na hitaji la mila na tamaduni. Hii inaonyesha udhibiti wa mawazo hata kama amesomea ughaibuni. Mwandishi anatuelezea:

> *Tom aliamua kujijengea nyumba kwao, nyumba moja nzuri ya wastani. Unaweza kulimbika mali na kutafahari jijini, lakini kama hujajijengea nyumba kijijini, watu wa kwetu watakuona kama fukara huna hunani, ukiulizwa huungami. Ndiyo mila ya kwetu. Sio Wakorosho, sio Wakanju na pia makabila mengine mengi Kiwachema, wanaamini hivyo. Kwa hiyo Tom alisifiwa na wote kijijini kwa kuwa mtamaduni (uk. 80-81).*

Akida alipopiga ripoti Kituo cha Polisi cha Kati ya Jiji, hakuhukumiwa bali aliachiliwa huru na kuonywa asiwahi fanya kosa lingine. Aliporejea pale Mtaa wa Falkland, baadaye vijana wanamwandama mpaka kwa Tim. Ujanja wa Tamari ulimwokoa na baadaye usiku wakafululiza mwendo hadi kwa kina Pam kujificha. Kwa bahati mbaya, shangaziye Pam aliporejea kutoka zamu ya usiku maana alikuwa muuguzi hakuridhika na badala yake akamfukuza Akida. Suluhu ya mwisho akawa bawabu Toili wa pale shangaziye Pam. Toili akawa mwokozi wa Akida hadi alipogura kwenda Canada kufadhiliwa kisomo na Tom Mangala. Udhibiti wa mawazo ulimnyima uhuru kwao Kiwachema na karibu umwangamize.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Mtima anaelezea jinsi Waafrika wenzake walivyojitenga naye pale ughaibuni. Utengano huu ulizuka kutokana na jinsi bado mawazo ya Waafrika yalivyodhibitiwa na kasumba za

ukolonizilizosheheni ubaguzi. Mtima anaeleza:

> *Nilipowaona sura zao, nilijua kuwa walikuwa watu wa nyumbani. Nadhani walinitambua pia kwani mtu wa nyumbani hafichiki, labda walikwishaniona jinsi nilivyojikunyata na kujitenga na kuwapuuza. (Uk. 79)*

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* suala la wenye nguvu ni walio na uwezo wa kudhibiti. Suala hili linamtawala Ndi- akilini mwake. Anatueleza:

> *Siku hizi kusema kweli ulimwengu hautawaliwi kamwe na wenye akili. Wenye nguvu za utawala, si wenye akili tena. Ni wenye mali na pesa na nguvu za kijeshi. Hao ndio wanaohodhi utaratibu wa maisha, nyenzo za mawasiliano, elimu, sayansi, teknolojia, dini, usafi na uchafu wa mazingira yetu. Aaaa, ni nguvu, nguvu na kudhibiti ndio utashi mkubwa wa mwanadamu sasa! (uk. 47)*

Mzungu huyu anatuonyesha jinsi wamedhibiti bara la Afrika na kutufyonza hata kiakili. Wametudhibiti mawazo na kututeka kwa anasa za maangamizi.

> *... "Sisi ndio tuliopewa haki ya kuudhibiti ulimwengu,"nikawahi kumsikia Mzungu mmoja akisema..."Tulipoona haitoshi Ulaya na mabara ya Mungu matupu duniani; na watu wasiofahamu faida ya ardhi kama nyinyi mmeikalia kivivu, tulikuja kuing'wapura!" ...Ndiyo..Ndiyo..."aliendelea yule Mzungu. "Akili zetu ndizo zilizotupa haki tutawale. Nguvu na ubora wetu wa kimaumbile ndio uliotuwezesha kujitawaza. Inafaa mshukuru kukufanyieni mengi katika kujifanyia sisi wenyewe. Sasa mwangaza umezagaa Afrika." (uk. 126).*

Usasa baadaye na utandawazi vinatamalaki dunia. Ndi- anapoogelea katika bahari ya ghafla iliyosababishwa na vua la mafuriko anaona unyonyaji unavozidi kwetu barani Afrika. Kwao kunzaidia kujaa, kwetu kutupu kabisa. Tumedhibitiwa kimawazo, kimuundo na kimaeneo. Ndi- anatueleza:

> *...maisha yanakwenda mbio ya ajabu. Kasi, kasi, kasi ya umeme iliyoanzishwa kwenye kiwanda cha Ford, Microsoft na MvIntosh. Ukifumbua macho utaona picha ya wenye mfumo huu wakiwa katika chombo fulani cha ajabu wakiwasukuma na kuwalazimisha watu wengine kudandia chombo chao. Kasi, kasi, kasi! Wenye puumzi bado wanamudu. Wasio na pumzi wanaangamia katika kudandia. Wanatengwa na kutupwa vibaya njiani huku bado wanang'anga'ania kusukuma chombo cha watu wengine – chombo cha waungwana. Tazama mgawiko huu: dunia ya kwanza, ya pili na ya tatu. (uk. 171)*

Katika riwaya ya *Chozi La Heri,* Dickson alitii amri ya Buda mwajiri wake. Msimulizi anasema:

> *...na asiwe vipi mwanagenzi, kinda wa miaka kumi kuingizwa katika biashara ya aina hii? Zipoasiku alipotetemeka nusura ajisaliti. Lakini alizoea kujipa moyo. Kila mara alipopatwa na kiwewe alijiambia, "Dickson, wewe jikaze,. Mzee wako hayupo hapa, amejipumzikia ahera. Na mama yako hakuwapo tangu hapo. Angekuwapo asingekuacha kutimbwa na ulitima." (uk. 119)*

Mama yake Dick amewatoroka na Dick amelanguliwa na kijakazi kwa tajiri mmoja wa dawa za kulevya. Ilimlazimu kutii kulangua dawa licha ya umri wake mdogo wa miaka kumi.

Mwandishi anatuelezea kisa cha mgonjwa mmoja kupitia kwa mhusika Selume aliyeitwa Tuama. Tuama anashikilia imani kuwa mila ni muhimu na kuonyesha kuwa amedhibitiwa kimawazo, ndiposa alitoroka kwao kupashwa tohara na kupata kupoteza damu nyingi sana hata kama baba yake mzazi alikuwa amelipinga jambo hilo. Tuama alisema:

> *"Kupashwa tohara si mila iliyopitwa na wakati. Bila tohara mwanamke hubakia kuwa mtoto. Nisingepashwa tohara nisingeolewa. Msiba uliowapata wenzangu ni bahati mbaya tu," ..."Lakini kupashwa tohara hakumaanishi kuacha shule. Dadangu, Tamira, alipashwa tohara lakini sasa amehitimu shahada katika chuo kikuu. La muhimu ni mtu kujifocus kwenye malengo yake tu. Mimi najua kwamba japo nimepashwa tohara, baada ya kupona uwele huu, nitaendelea na masomo yangu,"(uk. 144).*

### 4.1.9 Uchafuzi wa Mazingira

Mandhari ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira husawiriwa na matokeo yake kuwa maafa ya asili, kuharibu maisha ya watu na kuzua matatizo ya kibinadamu. Jamii huathirika na tabianchi au uharibifu wa mazingira. Athari ya mabadiliko ya tabianchi na upungufu wa raslimali kama maji, chakula na hewa safi ambavyo husababisha mizozo na vita vya kiuchumi.

Katika riwaya ya *Kufa Kuzikana,* Akida anaeleza mandhari aliyokumbana nayo njiani kuelekea alikohamia Tim. Ni wazi kuwa kuna uchafuzi wa mazingira wa hali ya juu. Akida anatueleza:

> *Tope lilijaa kwenye vijia vilivyokuwa baina ya mabanda hayo yaliyoinamiana. Fondogoo ya marundo ya taka zilizotota maji ya mvua na mikojo ya watu, ilichangamana na harufu ya vinyesi vya watoto na watu wazima vikaunda mseto wa mnuko mbaya, mbaya sana. ...Tukatokea kwenye uwanja mpana uliojaa marundo ya taka; si makopo, si karatasi, si kondomu zilizotumika tayari, si mifupa. Mbwakoko kadhaa na pakashume walizozania mabaki ya vyakula vilivyooza na kuozeana. Pembeni mwa uwanja huo, watoto – wavulana kwa wasichana, watu wazima –wanaume kwa wanawake, walichuchumaa kwa 'shughuli rasmi' ya kwenda uani peupe. ...''Waliochimba vyoo wanalipisha,'' (uk. 110-111).*

Hali hii inadhihirisha wazi jinsi mazingira yalivyochafuliwa na takataka zilitupwa ovyoovyo kila mahali.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Ndi- anatuelezea mazingira machafu pale barazani alikoenda:

> *Vinyesi vya watu na wanyama vinachekelea. Tope zisizokauka kama pua ya ng'ombe zinanyekenya. Vyote hivi vinagongana na ghasia, fujo na ugomvi. ...wenyewe huuita mtaa huu 'Kinyesini-jina la siridhariri. (uk. 32)*

Mvua kubwa ilinyesha na ikawa mafuriko. Mafuriko yalisababisha madhara mengi kwa ardhi na hata mijengo. Ndi- anatueleza:

> *Na maji yalipofika ardhini, yalifanya mikondo mikubwa yenye nguvu utadhani ile ya Nungwi. Na mkondo ukakumba kila kitu kilichothubutu kusimama njiani mwake: vibanda, nyumba, majumba, magari, baiskeli, watu... Waliyaita mafuriko ya ajabu!...upande wa pili, Maisha yakapoteza maana. Yakapoteza thamani! (uk. 165-166)*

Mwandishi anatuchorea hali jinsi ilivyo uwanja wa kago, mbali na mabaki ya chuma kuna uchafu mwingine ambao ni hatari kwa binadamu. Uliwaletea hali tata za kiafya. Anatukejeli kuwa sisi tunajua kutumia na bali sio kuunda teknolojia. Anasema:

> *Na, na, na, vyuma, vyuma, vyuma vimekuja kutupwa ovyo kutoka mbali. Na mbele zaidi mabaki ya madawa ya sumu ambayo yalihanikiza harufu iliyowaendesha chafya watu kila mara. ...ya mchanganyiko wa mafupa ya wanyama na watu waliokufa na kukaukia jangwani kwa ukame. ...Waafrika tunajua kutumia teknolojia tu! (uk. 87-188)*

Ridhaa anatueleza jinsi mazingira yalivyobadilika na kukosa uzuri baada ya vita vya kisiasa kuzuka Msitu wa Heri. Anasema:

> *Mizoga ya watu na wanyama, magofu na majumba yaliyoteketezwa kwa moto, na viunzi vya mimea iliyonyong'onyezwa na moto ilijikita kila mahali; uharibifu wa mali na mazingira ukashamiri. ...Magari yaliwaka moto bila kujali kilichomo ndani. Moshi ulipaa mbinguni katika mstari mmoja kama kwamba unakwenda kumshtakia Mungu (uk. 20-21)*

Mwandishi anatusimulia mandhari yalivyochafuliwa pale Msitu wa Mamba. Wakimbizi wakawa wengi na hitaji la kulima vyakula kukasababisha misitu kukatwa. Mwandishi anasema:

> *Matokeo ya uamuzi huu yalikuwa kukata miti kwa ajili ya kupata mashamba ya kupandia vyakula, na kwa ajili ya ujenzi; polepole mioshi ikaanza kuonekana ikifuka kutoka kwenye msitu ambao tangu hapo ulikuwa marufuku kwa binadamu (uk. 63).*

Mwandishi anazidi kuelezea jinsi uchafuzi wa mazingira ulivyoendelea hata baada ya wakimbizi kufurushwa kutoka Msitu wa Mamba katika awamu ya pili ya *Operesheni Rudi Edeni.* Mbao na makaa vilisafirishwa kutoka humo usiku. Mwandishi anasimulia:

> *Jambo la kushangaza ni kwamba, ingawa tulitangaziwa kuwa msitu huu ni marufuku kwa binadamu, usiku wa manane husikika milio ya malori na matrekta yakibeba shehena ya mbao, makaa na mahindi! Haijulikani ni wanyama gani wanaotekeleza haya, lakini hata ni mazoea ya msitu huu kufuka moshi mara kwa mara. Watu husema kwamba huenda hawa ni wachinja kafara ilhali wengine husema pengine ni bushfire! (uk. 77).*

## 4.0 Hitimisho

Utafiti huu ulihakiki riwaya tatu za Kiswahili *Kufa Kuzikana, Dunia Yao* na *Chozi la Heri* na kimahsusi ni kutoa maelezo ya kina hasa yaliyolenga maudhui, mtindo na mitazamo ya distopia yalishughulikiwa barabara. Tuliamua kuhakiki riwaya tatu pamoja kwa sababu zililenga mada yetu ya utafiti sawasawa. Usomi kwa riwaya hizi unaelezea masuala ya daistopia jinsi yanavyoathiri jamii ilhali jamii inaishi kwayo na kujikakamua. Jamii ndani ya riwaya hizo na hasa wahusika waliishi ndani ya hali hiyo ya uozo kutuonyesha kuwa walidhibitiwa na hali hizo.

Riwaya ya *Kufa Kuzikana* ilisawiri wahusika walioishi katika jamii iliyojaa ufisadi, ukabila, uongozi mbaya, matumizi ya pombe, umasikini, fujo na ghasia na hali nyingine nyingi kandamizi kwa maisha ya

binadamu. Kwa sababu hiyo, wahusika walionyesha hali ya kutamauka na hali hizo ngumu na kukosa uwezo wa kujiokoa kutokana na hali zao mbaya. Ukabila na machafuko ya kisiasa ndilo jambo kuu lililojitokeza na athari yake katika jamii na mazingira. Vita vya kikabila vilivyochochewa na siasa mbaya husababisha akina Akida kubakia yatima na kubahatisha kimaisha. Asingekuja kukutana na Tom, huenda Akida angebaki maskini hohehahe na kujifia.

Vita hivi vya kikabila, vilisababisha machafuko ya kimazingira, uharibifu wa mijengo na makazi ya binadamu na kusambaratisha familia nyingi sana. Mhusika Tom alimpoteza baba yake mzazi na karibu auwawe na mahasidi waliomuua baba alipoenda kumzika baba yake kijijini kwao. Mwishowe Tom anaamua kutorokea Canada na mkewe kwa sababu nyumbani hakukaliki tena. Rafikiye Akida, Tim naye alihangaika na maisha ya mjini Tandika na kufikia mwisho wa masimulizi mwandishi alituonyesha kuwa bado Tim alikuwa anaishi mtaa duni na maisha pale mjini yakiwa ya kubahatisha tu.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* hali za daistopia zilizosawiriwa katika riwaya hii zimesababishwa na mwandishi kutamaushwa na mustakabali wa bara la Afrika ambalo limezongwa na kila aina ya uozo kuanzia umaskini, uchafuzi wa mazingira, ukoloni mamboleo, ubinafsi, dhuluma dhidi ya binadamu na utandawazi. Mwandishi au msimulizi ametumia mhusika Ndi- kama kielelezo cha kuonyesha kuporomoka kwa bara la Afrika. Matukio yanayoshuhudiwa katika familia ya Ndi- yanalinganishwa na mataifa ya Kiafrika ambayo hupatwa na matatizo yanayotokana na wananchi wenyewe kwa kukosa kujielewa. Aidha wananchi huisahau na kuibeza asili yao huku wakiiga mambo ya kigeni kutoka kwa mataifa yaliyoendelea katika takribani kila nyanja ya kimaendeleo. Kutoshirikiana katika ujenzi wa taifa lao na kutojikomboa kimawazo huzua hali ya wasiwasi na maafa. Kulingana na mwandishi wa riwaya hii matatizo haya yanajitokeza katika uchumi, jamii, siasa na hata dini. Hivi kwamba, Mwafrika analo jukumu la kubadilika na wakati kwa kuzaliwa upya pamoja na jinsi ya kujiendeleza kimaisha.

Utafiti huu umebainisha kuwepo kwa uhusiano wa karibu baina ya mtindo na daistopia kimaudhui na kimtazamo. Kuzuka kwa utandawazi kumechangia kudhoofika kwa maadili katika jamii ya Kiafrika jambo ambalo limekuza katika muktadha wa kimtindo. Atari za utandawazi zimeshuhudiwa sio tu upande wa kuporomoka kwa maadili, bali hata katika itikadi za kisiasa zilizokopwa kiholela. Mifumo hiyo ya kigeni ya kisiasa inapwaya inapotumiwa katika muktadha wa Kiafrika. Bara la Afrika limekosa utambulisho na kujipata katika njia panda kiitikadi, kiuchumi, kisiasa, kidini na kijamii.

Riwaya hii inasawiri vijana ‘dunia yao’ yaani ulimwengu wa kifantasia ambamo wanaonekana kutojielewa, kudhibitiwa na nguvu fulani, kuasi asili yao pamoja na kuudharau utamaduni wao. Kutokana na uigaji wa utamaduni wa kimagaharibi, vijana wamekuwa watumwa katika bara la Afrika. hiki ni kinaya kuwa bara la Afrika lilipata uhuru na kujitawala. Baadhi ya vijana wamesawiriwa kama waliopoteza nguzo za utambulisho wao wa Kiafrika baada ya kuangamizwa ki-utamaduni huku maadili yao yakidhoofika kwa kujihusisha na uozo hususan matumizi ya dawa za kulevya, kutowajibika na kutowaheshimu wazee wao jambo ambalo limechangiwa sana na utandawazi. Baadhi wameambukizwa magonjwa ya zinaa na kuishi kutawaliwa na hofu.

Mwandishi huyu ameonyesha jinsi serikali zimedhibiti wananchi wake na kueneza mfumo wa ukandamizaji. Uhuru wa kibinafsi umepotea na unyonyaji wa rasilimali na kudidimizwa kimaendeleo kutokana na mfumo dhalimu wa soko huria. Tamaa ya uongozi, ufisadi, wizi wa kimabavu, ubakaji wa watoto wachanga umehalalishwa. Viongozi wametawaliwa na ubinafsi unaozua matabaka kadhaa. Wananchi wanaonekana kung’ang’ania masalio ya wenye nguvu pamoja na hali zao za umaskini.Vijana wamekosa nafasi za kazi kwa sababu lazima watoe rushwa au wawe na uhusiano wa karibu na wenye vyeo serikalini.

Mohamed anatumia mandhari ya daistopia katika kazi yake ili kusudia kutoa tahadhari na pia kutabiri hatari ijayo ya viongozi wasiowajibika, wanaotunga sera zisizostahili na matokeo ya kutodumisha haki za kibinadamu. Athari za ubinafsi na uporomokaji wa familia unadhihirika kutokana na familia ya Ndi-. Woga, udhibiti, kutamauka na uasi ndivyo wahusika wanajihusisha kila uchao angalau waendelee kuishi.

Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* mwandishi alitumia mtindo teule kuelezea distopia. Maudhui yakihakikiwa yaliyolenga daistopia nayo mitindo iliyojenga mada yetu kuwekwa wazi. Mitazamo iliyolenga mada iliwekwa wazi na kuelezewa kwa kina. Wahusika na mandhari ni vipengele muhimu vilivyochangia kufanikisha upataji wa data yetu ya utafiti.

## Marejeleo


Bibiana, S. (2014). *Trajectories Of Social Isolation.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Cha Indiana. (*Isiyochapishwa*).

Bradford, W. (2003). *Growth of Literature.* London: Kingsway Ltd.

Bryman, A. (2004). *Disneyization of Society*. London: Sage Publication Limited.

Buffon, G. (1930). *Buffon's Discourse on Style.* Paris Librairie: Hatier Publishers

Camus, F. (1984). *The Control of Man's Fate in The Stranger.* London: Salman Ltd.

Chacha, N.C. (1980). Ushairi wa Abdilatif. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Chepkwony, B. (2017). *A Literary Histographical Analysis of Kinyanjui Kombani's: The Last Villians of Molo*. Makala: *African Studies Journal PP 102-116.*

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style.* London: Longman Group Ltd.

Holman, C. H (1960). *A Handbook to Literature* (Revised and Enlarged). Salisbury: The Odyssey Press Inc.

Jackson, P. (1999). *Understanding West Literal works*. Dublin: Ireland Pub. Ltd.

Kehinde, A. (2004). *Post Independence Dissillusionment in Contemporary African Fiction*. Nairobi: Oxford University Press.

Kerlinger, F. (1969). *Research Myths: Statistics, Practicability and Status.* London: Taylor Press.

Kimani, N. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: University Press,

Kimani, N. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Sai Industries Limited.

Kimani, N. na Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kinoti, N. (2012). *Mtazamo wa Mwanasiasa wa Kiafrika Katika Ushairi.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kitula, K. (1999). *Language Development Research in the 21st Century*. Nairobi. JKF.

Kombo, D. & Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kruger, (1998). *Usawiri wa Mwanamke Kama Mhusika wa Fasihi*. Makala ya utafiti.

Leech, G & Short, M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to Fictional Prose.* London and New York: Longman.

Masinde, E. (1992). Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Matei, A. (2014). *Chozi La Heri.* Nairobi: One Planet Publishing & Media Services.

Marx, K. (2004). *Capital* Vol 1, *Afterwood to the Second German Edition*(4). Berlin: AGM.

Merriam, W (2003). *Merriam Webster Collegiate Dictionary.* London: Merriam Webster.

Mohamed, S. (2006 ). *Dunia Yao.* Nairobi: Oxford University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd. M. Press.

Mugambi, H. (1982). Fasihi yetu. Nairobi: OUP.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999). *Research Me*thods. Nairobi: Acts Press.

Mutua, J. M. (2017). Mitazamo ya Waandishi wa Kike na Kiume Kuhusu Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Pwani.

Mutwiri, G. (2005). Mitazamo ya Utendakazi wa Nyiso Katika Jamii ya Watigania. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Muhamed, B. (2011). Usemezano kama Mkakati wa Katika Fasihi Andishi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mukobwa, F. (1987). Kazi na Faida za Jamii. Nairobi: JKF.

Mungai, M. (2013). *Nairobi's Matatu Men*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Musangi, J. (2008). *A Walk Through the Criminal City*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Witwatersrand. Afrika Kusini: (Haijachapishwa)

Mwanje, I. J. (2001). *Qualitative Research Process: Social Science Research Methodology Series, Module 2*. Addis Ababa: OSSREA

Ndago, G. (2020). *Nationhood and Ethnic Ideology: examining selected Cartoons Paratextsin* Kwani? *Kiswahili.* Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).

Ngolo, E. K. (2011). Mabadiliko ya Kimtindo Katika Ushairi wa Said A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Odhiambo, T. (2004). *(Un)popularity of Popular Literature in Kenya: The case of David Maillu*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Witwatersrand. (Isiyochapishwa). ______(2010). *The Postcolonial City*. Makala mtandaoni.

Oiko, F. (2017). *Uhakiki wa Kimtindo Katika Tamthlia za Arege*. Chuo Kikuu cha Maasai Mara. Tasnifu ya Uzamili. (Iliyochapishwa).

Okwena, S. (2013). Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia za Arege. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Oxford, (1978). *Advanced Dictionary of English.* Oxford: OUP.

Ponera, A. (2019). Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu. Dar es Salaam: CTP.

Said, E. (1978). *Orientalism.* Newyork: Newyork Publishers.

Scholes, K. (1974). *Structuralism in Literature: An Introduction.* New York. YUP.

Senkoro, F.E.M.K (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

-----------(1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaaam: Press and Publicity Centre.

Syambo, K. na Mazrui A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Truex, D. (1996). *Theorizing in Information Systems Research*. Oxford: OUP.

Wafula, R. M. (1987). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2003). *Kufa Kuzikana.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: JKF.

_____________(2003*). Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers.

______________(2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications Limited.

______________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uhakiki na Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd

Woods, J.T. (1997). *Communication Theories In Action.* London: Wadsworth Publishing Company.